# القرآن الحكيم

# QURANI TAKATIFU

Swahili Quran Translation

by
Sheikh Abdullah Saleh Al-Farsy
(Former Chief Kadhi of
Zanzibar & Kenya)

اٰيَاتُهَا ١١١ (١٧) سُورَةُ بَنِيٓ إِسْرَآءِيلَ مَكِّيَّةٌ (٥٠) رُكُوعَاتُهَا ١٢

*Ina Aya 111* *Ina Makara 12*

# SURAT BANI ISRAIL

*(Imeteremka Makka)*

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

سُبْحٰنَ الَّذِيْٓ اَسْرٰى بِعَبْدِهٖ لَيْلًا مِّنَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ اِلَى الْمَسْجِدِ الْاَقْصَا الَّذِيْ بٰرَكْنَا حَوْلَهٗ لِنُرِيَهٗ مِنْ اٰيٰتِنَا ۭ اِنَّهٗ هُوَ السَّمِيْعُ الْبَصِيْرُ ①

1. Utukufu ni wake yeye ambaye alimpeleka mja wake usiku (mmoja tu) kutoka Msikiti Mtukufu (wa Makka) mpaka Msikiti wa mbali (wa Baytul Muqaddas-Falastini) ambao (tumeubariki na) tumevibariki vilivyoko pembezoni mwake (Tulimpeleka hivyo) ili tumuonyeshe baadhi ya Alama zetu. Hakika Yeye (Mwenyezi Mungu) ni Mwenye kusikia (na) Mwenye kuona.

وَاٰتَيْنَا مُوْسَى الْكِتٰبَ وَجَعَلْنٰهُ هُدًى لِّبَنِيْٓ اِسْرَاۗءِيْلَ اَلَّا تَتَّخِذُوْا مِنْ دُوْنِيْ وَكِيْلًا ②

2. Na tulimpa Musa Kitabu, na tukakifanya uongofu kwa Bani Israili (Mayahudi); (akawaambia Mwenyezi Mungu): "Msimfanye mlinzi (wenu kiumbe) badala Yangu.

---

1. Si ajabu Mwenyezi Mungu kumpeleka Mtume Wake kutoka Makka mpaka Shamu na akamrejesha katika baadhi ya saa za usiku huo huo na kumuonyesha aliyomuonyesha.

Leo binaadamu Mwenyezi Mungu amewawezesha haya ya kuzunguka ulimwengu mzima na kurejea kwa saa chache tu hivi. Na yote haya ni kwa ajili ya kuonyesha ukweli wa Qurani kuwa Qurani haisemi jambo, ikabainika kuwa jambo hilo ni uwongo. Muhali hayo kama alivyosema Mwenyezi Mungu na kama tunavyoona na tutakavyozidi kuona sisi na kuona watakaokuja baada yetu sisi na watakaokuja baada ya hao na baada ya hao na baada ya hao, mpaka ulimwengu umalizike kila saa na wakati utakuwa unadhihiri tu ukweli wa dini ya Kiislamu. Dini iliyonyoka kweli kweli.

Mwanzo tu wa Sura hii na katika Aya waliyoifanya kuwa ni ya 2 Makadiyani wametia ukafiri wa kusema kuwa safari ya Mtume kutoka Makka mpaka Baytul Muqaddas (Israil) ni njozi yaani ndoto si kwa kiwiliwili chake. Wameandika hivi:– "Pia inaitwa Israa kwa kuwa imeanza na habari ya Njozi kuu ya Mtume s.a.w., inayohusu safari ya Usiku aliyokwenda Jerusalem . . ." Na huu ni ukafiri dhahiri na kuipinga Qurani dhahiri shahir. Qurani imesema *Asraa Biabdihii* = Amempeleka mwenyewe mtumwa wake; haikusema:- *Asraa Biruhi Abdihi* = Ameipeleka roho ya mja wake (katika usingizi). Basi Itikadi hii ni yao si ya Kiislamu. Hapana madhehebu moja ya Kiislamu iliyosema hivi.

Yenye khitilafu ni *Miiraji* = Safari ya kutoka Baytul Muqaddas mpaka mbinguni. Hii ndiyo ambayo baadhi chache kabisa ya Waislamu wanasema ilikuwa kwa Roho bila ya kiwiliwili. Wala hawakusema kuwa ilikuwa kwa ndoto tu (njozi) kama wanavyosema wao kwa zote mbili. Na huko kusema: "Hivyo tunakuta ya kuwa Masahaba kadha wa kadha na baadhi ya wanavyuoni wa Kiislamu . . . wanasema kuwa Israa ni njozi." Wallahi! Watu hawa hawaamini Mwenyezi Mungu wala hawamuogopi, kwa uchu wao mkubwa uliowashika wa kutaka kuwatoa Waislamu katika Uislamu wao. Wallahi hakuna Sahaba hata mmoja aliyesema kuwa Israa ni ndoto. *Laanatul Lahi Alaal Kaadhibyn* = Laana ya Mwenyezi Mungu itawashukia wazuaji. Hao Masahaba na wanavyuoni waliosema kwa Roho (sio Ndoto) ni katika Miiraji si Israa. Tena ni wachache kabisa — hata 10 hawatimii. Na wanajua, ila wanataka kuwapoteza tu Waislamu. Na huko kujidai kumtaja Ibn Jarir na Ibn Is-haq na Addurarul Manthur na Hisham na Maadi . . . kuwa hao wametaja kuwa Masahaba na baadhi ya wanavyuoni wamesema Israa ilikuwa katika ndoto, ni uwongo kabisa; hawakutaja haya kabisa; wala hawakutaja pia majina ya Masahaba kadha wa kadha na baadhi ya wanavyuoni waliosema Miiraji ni ndoto. Uwongo kabisa. Hakuna viumbe wasiomuogopa Mwenyezi Mungu katika kupoteza watu kuliko hawa! Silaha mbaya kabisa wanayoitumia katika kupoteza Waislamu. Silaha ya kumsingizia uwongo Mwenyezi Mungu na Mtume na wanavyuoni, na kutaja vitabu na juzuu

3. (Na pia akawaambia) "Enyi kizazi cha wale tuliowapandisha (katika jahazi) pamoja na Nuhu! (kuweni wenye shukrani kama mzee wenu huyo). Hakika yeye alikuwa mja mwenye shukrani."

ذُرِّيَّةَ مَنْ حَمَلْنَا مَعَ نُوحٍ ۚ إِنَّهُ كَانَ عَبْدًا شَكُورًا ﴿٣﴾

4. Na tukawafunulia Bani Israili katika (hicho) Kitabu (chao kuwa): "Bila shaka nyinyi mtafanya uharibifu katika nchi mara mbili, na kwa yakini mtatakabari kutakabari kukubwa."

وَقَضَيْنَآ إِلَىٰ بَنِيٓ إِسْرَآءِيلَ فِي الْكِتٰبِ
لَتُفْسِدُنَّ فِي الْأَرْضِ مَرَّتَيْنِ وَلَتَعْلُنَّ
عُلُوًّا كَبِيرًا ﴿٤﴾

5. "Basi itapofika ahadi ya (kulipwa kwa ajili ya uharibifu wa) kwanza wa hiyo miharibifu miwili, tutakuleteeni watu wetu wenye mapigano makali; nao wataingia mijini mwenu kila upande. Na hii itakuwa ni ahadi itakayotimizwa." (Tutakuadhibuni tu maadamu mtafanya fisadi).

فَإِذَا جَآءَ وَعْدُ أُولٰىهُمَا بَعَثْنَا عَلَيْكُمْ عِبَادًا لَّنَآ أُولِي
بَأْسٍ شَدِيدٍ فَجَاسُوا خِلٰلَ الدِّيَارِ ۚ وَكَانَ
وَعْدًا مَّفْعُولًا ﴿٥﴾

6. "Kisha tutakurudisheni nguvu zenu juu yao (hao waliokushindeni), na tukuongezeeni mali na watoto na tutakufanyeni wenye kundi kubwa kuliko wao."

ثُمَّ رَدَدْنَا لَكُمُ الْكَرَّةَ عَلَيْهِمْ وَأَمْدَدْنٰكُم بِأَمْوٰلٍ
وَبَنِينَ وَجَعَلْنٰكُمْ أَكْثَرَ نَفِيرًا ﴿٦﴾

7. "Basi mkifanya wema, mnajifanyia wenyewe nafsi zenu; na mkifanya ubaya, mnajifanyia nafsi zenu wenyewe. Na itapofika ahadi ya (malipo ya uharibifu wa) mwisho (tutakuleteeni watu wenye nguvu vile vile) ili wazidhalilishe nyuso zenu, na wauingie Msikiti kama walivyouingia mara ya kwanza. Na waharibu kuharibu kukubwa kabisa muda wa kukutawalieni."

إِنْ أَحْسَنتُمْ أَحْسَنتُمْ لِأَنفُسِكُمْ ۖ وَإِنْ أَسَأْتُمْ فَلَهَا ۚ
فَإِذَا جَآءَ وَعْدُ الْاٰخِرَةِ لِيَسُۥٓـُٔوا وُجُوهَكُمْ وَلِيَدْخُلُوا
الْمَسْجِدَ كَمَا دَخَلُوهُ أَوَّلَ مَرَّةٍ وَلِيُتَبِّرُوا مَا عَلَوْا
تَتْبِيرًا ﴿٧﴾

8. (Lakini mkitengenea) huwenda Mola wenu akakurehemuni; na kama mtarudia (mwendo wenu wa kuharibu, Sisi pia) tutarudia (kukuangamizeni)." Na tumeifanya Jahanamu ni gereza kwa ajili ya makafiri.

عَسَىٰ رَبُّكُمْ أَن يَرْحَمَكُمْ ۚ وَإِنْ عُدتُّمْ عُدْنَا ۘ
وَجَعَلْنَا جَهَنَّمَ لِلْكٰفِرِينَ حَصِيرًا ﴿٨﴾

9. Hakika hii Qurani inaongoza katika njia iliyonyoka kabisa; na inawapa habari njema Waislamu wafanyao vitendo vizuri, ya kwamba watapata malipo makubwa (kabisa).

إِنَّ هٰذَا الْقُرْءَانَ يَهْدِي لِلَّتِي هِيَ أَقْوَمُ وَيُبَشِّرُ
الْمُؤْمِنِينَ الَّذِينَ يَعْمَلُونَ الصّٰلِحٰتِ أَنَّ لَهُمْ
أَجْرًا كَبِيرًا ﴿٩﴾

10. Na (inatoa khabari) kwamba wale wasioamini Akhera tumewaandalia adhabu inayoumiza kabisa.

وَأَنَّ الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِالْاٰخِرَةِ أَعْتَدْنَا لَهُمْ عَذَابًا
أَلِيمًا ﴿١٠﴾

---

zake na sahifa zake — na hali ya kuwa ni uwongo kabisa, hamna humo hayo wayasemayo. Hii balaa kubwa iliyowashukia Waislamu isiyokuwa na mfano. *Nasrum Minallahi Wafat-hun Qaryb, Inshallah.*

3. Binaadamu wote waliokuja ulimwenguni baada ya Nabii Nuhu ni kizazi cha wale watoto wa Nabii Nuhu waliokuwa jahazini siku ile; wakaokoka.

5-8. Yote haya yamewafika Mayahudi na yatazidi kuwafika maadamu hawatasilimu wakenda mwendo mzuri. Na huku kushinda kwao kwa myaka hii ni kwa ajili ya kusaidiwa na dola za Amerika na Ulaya. Na haya ndiyo aliyoyasema Mwenyezi Mungu katika aya ya 112 ya *Surat Aali Imran*. Wakiwaacha mkono hao basi wamekwisha kulala Mayahudi.

7. Katika aya waliyoifanya ya 8 wametia ukafiri wao wa kusema kuwa Nabii Isa amesulubiwa. Na tumerejeza ukafiri wao huu katika marejezo ya Aya ya 54 ya Sura ya *Aali Imran*.

11. Na mwanadamu huomba shari kama vile aombavyo kheri; kwani mwanadamu ni mwenye pupa (kutaka jambo).

وَيَدْعُ الْإِنسَانُ بِالشَّرِّ دُعَاءَهُ بِالْخَيْرِ ۖ وَ
كَانَ الْإِنسَانُ عَجُولًا ﴿١١﴾

12. Na tumefanya usiku na mchana kuwa ishara mbili (za uweza wetu). Kisha tumeifuta (tumeiondoshea mwangaza) ishara ya usiku; na tukaifanya ishara ya mchana ni yenye mwangaza, ili mtafute fadhila itokayo kwa Mola wenu (hapo mchana), na mpate kujua idadi ya myaka na hisabu (nyingine). Na kila kitu (kinachohitajika katika dini na dunia) tumekieleza waziwazi (humu katika Qurani).

وَجَعَلْنَا اللَّيْلَ وَالنَّهَارَ آيَتَيْنِ ۖ فَمَحَوْنَا آيَةَ اللَّيْلِ
وَجَعَلْنَا آيَةَ النَّهَارِ مُبْصِرَةً لِّتَبْتَغُوا فَضْلًا مِّن
رَّبِّكُمْ وَلِتَعْلَمُوا عَدَدَ السِّنِينَ وَالْحِسَابَ ۚ وَكُلَّ
شَيْءٍ فَصَّلْنَاهُ تَفْصِيلًا ﴿١٢﴾

13. Na kila mwanaadamu tumemfungia (jaza ya) vitendo vyake shingoni mwake; na tutamtolea siku ya Kiama daftari (iliyoandikwa ndani yake kila alilolifanya) atakayoikuta imekunjuliwa (aambiwe):

وَكُلَّ إِنسَانٍ أَلْزَمْنَاهُ طَائِرَهُ فِي عُنُقِهِ ۖ وَنُخْرِجُ
لَهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ كِتَابًا يَلْقَاهُ مَنشُورًا ﴿١٣﴾

14. "Soma daftari yako. Nafsi yako inakutosha leo kukuhisabu."

اقْرَأْ كِتَابَكَ كَفَىٰ بِنَفْسِكَ الْيَوْمَ عَلَيْكَ حَسِيبًا ﴿١٤﴾

15. Anayeongoka, basi anaongoka kwa maslaha ya nafsi yake mwenyewe, na anayepotea, basi anapotea kwa khasara (ya nafsi) yake mwenyewe. Wala hatabeba mbebaji mzigo wa mwingine. Na sisi si wenye kuwaadhibisha (viumbe) mpaka tuwapelekee Mtume (awafahamishe yaliyo ya haki. Basi wakiyakataa ndipo wanapoangamizwa).

مَّنِ اهْتَدَىٰ فَإِنَّمَا يَهْتَدِي لِنَفْسِهِ ۖ وَمَن ضَلَّ
فَإِنَّمَا يَضِلُّ عَلَيْهَا ۚ وَلَا تَزِرُ وَازِرَةٌ وِزْرَ أُخْرَىٰ ۗ
وَمَا كُنَّا مُعَذِّبِينَ حَتَّىٰ نَبْعَثَ رَسُولًا ﴿١٥﴾

16. Na tunapotaka kuuangamiza mji (kwa kuwa watu wake wanafanya mabaya) tunawaamrisha (hao) mafisadi wake (waache ubaya); lakini wanaendelea na maasiya yao humo. Hapo kauli (ya kuadhibiwa) inathubutu juu yake (mji huo) na tunauangamiza maangamizo makubwa.

وَإِذَا أَرَدْنَا أَن نُّهْلِكَ قَرْيَةً أَمَرْنَا مُتْرَفِيهَا
فَفَسَقُوا فِيهَا فَحَقَّ عَلَيْهَا الْقَوْلُ فَدَمَّرْنَاهَا
تَدْمِيرًا ﴿١٦﴾

17. Na karne ngapi tumeziangamiza baada ya Nuhu! Na Mola wako anatosha kwa dhambi za waja wake kuwa Mwenye kuzijua, Mwenye kuziona, (basi atawalipa tu).

وَكَمْ أَهْلَكْنَا مِنَ الْقُرُونِ مِن بَعْدِ نُوحٍ ۗ
وَكَفَىٰ بِرَبِّكَ بِذُنُوبِ عِبَادِهِ خَبِيرًا بَصِيرًا ﴿١٧﴾

---

11. Binaadamu akifikwa na misukosuko mara hujitakia hata kufa kumtike. Nayo sivyo hivyo. Ulimwengu ndiyo kama hivi tunavyouona — dhiki baada ya faraji na faraji baada ya dhiki na vivi hivi.

Aya hii wameipindua maelezo yake. Ati wanadai kuwa mtu hajiapizi mwenyewe. Mtu anajiua mwenyewe, itakuwa kujiapiza? Mara ngapi watu wanaomba "Eee Mwenyezi Mungu! Nifishe, kuliko maisha haya."

12. Zinatajwa baadhi ya faida za kupatikana mchana na usiku.

15. Hapa ni mahala pamoja pa kuwajibu wale wanaosema "Mwana wa haramu hana kheri. Hata akifanya wema hatatiwa Pepo ya Mungu; atatiwa Pepo ya Shaddad . . ."

Ana kosa gani huyo hata yamfike haya! Wenye makosa ni hao waliomzaa kwa njia ya haramu, siye yeye. Na dhambi za mtu mwengine—kama ilivyosemwa hapa—hachukui mtu mwengine. Basi maneno hayo wanayoyasema ni uwongo kabisa. Wala hakuna pepo ya Shaddad wala Adi wala nani. Pepo ni ya Mwenyezi Mungu tu. Wasiseme watu wasiyoyajua. Katika mahala mlimobainishiwa uwongo wa maneno hayo—ya kuwa Mwanaharamu haingii Peponi-ni sahifa 256 ya *Asnal Matalibfy Ahadythi Mukhtalifatil Maratib;* na sahifa 182 na 192 za *Tam-yizatul Tayyib Minal Khabyth Fymaa Yaduru Alal Alsinati Minal Hadythi,* na sahifa 101 ya *Al Luu luil Marsuu* na kwengineko.

18. Anayetaka (starehe za dunia hii) ipitayo upesi (wala hana haja ya akhera), basi tutampa upesiupesi humo, (lakini) tunayoyataka; (tena) kwa yule tumtakaye; kisha tumemfanyia Jahanamu; ataingia humo, hali ya kuwa ni mwenye kudharauliwa na kufukuzwa (huku na huku).

مَنْ كَانَ يُرِيدُ الْعَاجِلَةَ عَجَّلْنَا لَهُ فِيهَا مَا نَشَاءُ لِمَنْ نُرِيدُ ثُمَّ جَعَلْنَا لَهُ جَهَنَّمَ يَصْلَاهَا مَذْمُومًا مَدْحُورًا ﴿١٨﴾

19. Na anayetaka akhera na akazifanyia jitihada amali zake, na hali ya kuwa ni Mwislamu, basi hao jitihada yao (hiyo) itakuwa ni yenye kushukuriwa.

وَمَنْ أَرَادَ الْآخِرَةَ وَسَعَىٰ لَهَا سَعْيَهَا وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَأُولَٰئِكَ كَانَ سَعْيُهُمْ مَشْكُورًا ﴿١٩﴾

20. Wote hao (wema na wabaya) tunawapa—hawa na hawa—katika atia (kipawa) za Mola wako; na atia za Mola wako hazizuiliki (kumfikia kiumbe chake).

كُلًّا نُمِدُّ هَٰؤُلَاءِ وَهَٰؤُلَاءِ مِنْ عَطَاءِ رَبِّكَ ۚ وَمَا كَانَ عَطَاءُ رَبِّكَ مَحْظُورًا ﴿٢٠﴾

21. Tazama jinsi tulivyowafadhilisha (hapa duniani) baadhi yao (viumbe) kuliko wengine; na bila shaka akhera ni yenye vyeo vikubwa zaidi, na vyenye kufadhiliana zaidi (pia).

انْظُرْ كَيْفَ فَضَّلْنَا بَعْضَهُمْ عَلَىٰ بَعْضٍ ۚ وَلَلْآخِرَةُ أَكْبَرُ دَرَجَاتٍ وَأَكْبَرُ تَفْضِيلًا ﴿٢١﴾

22. Usifanye mungu mwingine pamoja na Mwenyezi Mungu; usije ukawa mwenye kulaumiwa (na) mwenye kukosa wa kukunusuru.

لَا تَجْعَلْ مَعَ اللَّهِ إِلَٰهًا آخَرَ فَتَقْعُدَ مَذْمُومًا مَخْذُولًا ﴿٢٢﴾

23. Na Mola wako amehukumu kuwa msimuabudu yoyote ila Yeye tu. Na (ameagiza)kuwafanyia wema (mkubwa) wazazi. Kama mmoja wao akifikia uzee, (naye yuko) pamoja nawe, au wote wawili, basi usiwaambie hata Ah! Wala usiwakemee. Na useme nao kwa msemo wa hishima (kabisa).

وَقَضَىٰ رَبُّكَ أَلَّا تَعْبُدُوا إِلَّا إِيَّاهُ وَبِالْوَالِدَيْنِ إِحْسَانًا ۚ إِمَّا يَبْلُغَنَّ عِنْدَكَ الْكِبَرَ أَحَدُهُمَا أَوْ كِلَاهُمَا فَلَا تَقُلْ لَهُمَا أُفٍّ وَلَا تَنْهَرْهُمَا وَقُلْ لَهُمَا قَوْلًا كَرِيمًا ﴿٢٣﴾

24. Na uwainamishie bawa la unyenyekevu kwa (njia ya kuwaonea) huruma (kwa kuwaona wamekuwa wazee). Na useme: "Mola wangu! Warehemu (wazee wangu) kama walivyonilea katika utoto."

وَاخْفِضْ لَهُمَا جَنَاحَ الذُّلِّ مِنَ الرَّحْمَةِ وَقُلْ رَبِّ ارْحَمْهُمَا كَمَا رَبَّيَانِي صَغِيرًا ﴿٢٤﴾

25. Mola wenu anajua sana yaliyo nyoyoni mwenu. Kama mkiwa wema (kwa wazee wenu daima; lakini mara moja mbili hivi mkapotea, basi Mungu atakusameheni) kwani Yeye ni Mwenye kuwaghufiria wenye kurejea (kwake).

رَبُّكُمْ أَعْلَمُ بِمَا فِي نُفُوسِكُمْ ۚ إِنْ تَكُونُوا صَالِحِينَ فَإِنَّهُ كَانَ لِلْأَوَّابِينَ غَفُورًا ﴿٢٥﴾

26. Na umpe jamaa (yako) haki yake, na maskini na msafiri aliyeharibikiwa, wala usitawanye (mali yako) kwa ubadhirifu.

وَآتِ ذَا الْقُرْبَىٰ حَقَّهُ وَالْمِسْكِينَ وَابْنَ السَّبِيلِ وَلَا تُبَذِّرْ تَبْذِيرًا ﴿٢٦﴾

---

Bali imekuja Hadithi Sahihi khasa kuwa Mtume kasema kwamba Mwanaharamu hazimkhusu kitu dhambi za wazee wake; kama ilivyo katika sahifa 228 ya juzuu ya 2 ya *Tanzy hush Shary-atil Marfua Anıı akhbarish Shaniy-atil Mawdhua.*

16. Tumebainisha katika Aya ya 123 ya *Suratul An-am* kuwa hao wakubwa huwa mafisadi, mambo yakaharibika na adhabu ikashuka.

19. Akhera huwezi kuipata mpaka uifanyie amali zake, ndipo uipate. Ukiona vinaelea vinaundwa. Mtaka cha mvunguni huinama.

إِنَّ الْمُبَذِّرِينَ كَانُوا إِخْوَانَ الشَّيَاطِينِ ۖ وَكَانَ
الشَّيْطَانُ لِرَبِّهِ كَفُورًا ﴿٢٧﴾

27. Hakika watumiao kwa ubadhirifu ni ndugu wa mashetani (wanamfuata Shetani). Na Shetani ni mwenye kumkufuru Mola wake.

وَإِمَّا تُعْرِضَنَّ عَنْهُمُ ابْتِغَاءَ رَحْمَةٍ مِّن رَّبِّكَ تَرْجُوهَا
فَقُل لَّهُمْ قَوْلًا مَّيْسُورًا ﴿٢٨﴾

28. Na kama (unajipurukusha) nao (sasa hivi kwa kuwa huna kitu) lakini unatafuta rehema ya Mola wako (riziki) unayoitumai, basi sema nao maneno laini (ya kuwapa waadi ya kuwa ukipata utawapa).

وَلَا تَجْعَلْ يَدَكَ مَغْلُولَةً إِلَىٰ عُنُقِكَ وَلَا تَبْسُطْهَا
كُلَّ الْبَسْطِ فَتَقْعُدَ مَلُومًا مَّحْسُورًا ﴿٢٩﴾

29. Wala usifanye mkono wako (kama) uliofungwa shingoni mwako, wala usiukunjue ovyo ovyo, utakuwa ni mwenye kulaumiwa (ukifanya hivyo) na kufilisika (ukiukunjua ovyo ovyo).

إِنَّ رَبَّكَ يَبْسُطُ الرِّزْقَ لِمَن يَشَاءُ وَيَقْدِرُ ۚ إِنَّهُ كَانَ
بِعِبَادِهِ خَبِيرًا بَصِيرًا ﴿٣٠﴾ ع

30. Hakika Mola wako humkunjulia riziki amtakaye na humdhikishia (amtakaye). Hakika Yeye kwa waja wake ni Mwenye kuwajua na kuwaona; (anajua yupi anayestahiki utajiri na yupi anayestahiki ufakiri).

وَلَا تَقْتُلُوا أَوْلَادَكُمْ خَشْيَةَ إِمْلَاقٍ ۖ نَّحْنُ نَرْزُقُهُمْ
وَإِيَّاكُمْ ۚ إِنَّ قَتْلَهُمْ كَانَ خِطْئًا كَبِيرًا ﴿٣١﴾

31. Wala msiwaue watoto wenu kwa kuogopa umasikini. Sisi ndio tunaowaruzuku wao na nyinyi (pia). Kwa yakini kuwaua ni khatia kubwa.

وَلَا تَقْرَبُوا الزِّنَىٰ ۖ إِنَّهُ كَانَ فَاحِشَةً وَسَاءَ سَبِيلًا ﴿٣٢﴾

32. Wala mskikaribie zinaa. Hakika hiyo (zinaa) ni uchafu (mkubwa) na ni njia mbaya (kabisa).

وَلَا تَقْتُلُوا النَّفْسَ الَّتِي حَرَّمَ اللَّهُ إِلَّا بِالْحَقِّ ۗ وَمَن
قُتِلَ مَظْلُومًا فَقَدْ جَعَلْنَا لِوَلِيِّهِ سُلْطَانًا فَلَا

33. Wala msiue nafsi ambayo Mwenyezi Mungu amekataza (kuiua) isipokuwa kwa haki (Akahukumu Hakimu kuwa mtu huyo anastahiki kuuawa na akatoa amri ya kuuawa). Na mwenye

---

20. Ama riziki ya hapa duniani, wote wanapewa: wema na wabaya.

Huna umkataaye — Kafiri kwa Isilamu
Hakuna umuwachaye — Waturuzuku dawamu
Ya wasial karamu — Iwe kun Fayakunu.

21. Basi tushughulike tupate hayo.

22-39. Katika uwongozi mkubwa uliyoko katika Qurani unaopasa kufuata kweli kweli, kama kila uwongozi mwingine uliomo humo na katika Hadithi za Mtume. Anayetengenea atatengenekewa tu duniani na Akhera.

29. Kila kitu kiwe sawa sawa; Usimili upande huu wala upande ule. Iwe kama mizani.

31. Hapo kabla ya Uislamu walikuwa wanawazika wazima wazima watoto wao; ima kwa kuchelea kufanya ya aibu (wakiwa wanawake) au kwa ajili ya kushindwa au kuogopa kushindwa na khasara za kuwalisha na kuwavika.

Sasa kuna wengine wanayoyafanya hayo ya kuwabigija roho mpaka wakafa hao Malaika wa Mungu inapokuwa wanawazaa kwa haramu. Basi dhambi juu ya dhambi—dhambi za kuzini na za kuwaua hao watoto. Na dhambi hizo wanazigawanya wote wawili — huyo mwanamke na huyo mwanamume.

Na kuiharibu mimba kwa ajili ya kuchelea aibu ya kuzaa mwanaharamu kunakurubiana na huko kuwabigija roho wakishazaliwa. Mwenye kuua jaza yake ni Moto tu kama anavyosema Mwenyezi Mungu katika Aya ya 93 ya *Suratin Nisaa.*

Na kunaingia katika kuua watoto Kutowalea kwa Vizuri. Kutowapa mafundisho ya dini yao na mafundisho ya Dunia. Ukitomfanyia mwanao haya ndiyo umemuua hivyo. Ni wajibu wa kila mzee kumtengenezea mwanawe haya na yaliyo kama haya.

Katika Aya hii waliyoifanya kuwa ni ya 32 wamesema uwongo katika maelezo yao. Makusudio ya Aya hiyo ni kukataza ule mwendo mbaya waliokuwa nao Waarabu wa KUUA watoto wao kwa ajili ya kuogopa aibu na njaa. Wanajua kuwa mpaka sasa wako watu wanaofanya haya. Miongoni mwa hao ni wale wanaozaa kwa haramu wakaogopa aibu. Mara ngapi wanawabigija koo, wakawaua papo hapo!

33. Ama huku kuua kweli kweli mambo yanazidi. Ni moto tu wa milele huko Akhera.

يُسْرِف فِّي الْقَتْلِ ۖ إِنَّهُ كَانَ مَنصُورًا ﴿٣٣﴾

kuuawa kwa kudhulumiwa, basi tumempa nguvu mrithi wake (juu ya muuaji huyo, akitaka ataomba kwa Hakimu kuwa amuuwe kama alivyomuuwa mtu wake na akitaka atamsamehe na akitaka atamtoza kitu.) Basi (huyo mrithi asifanye fujo katika kuua kwa ajili ya huyo mtu wake aliyeuliwa). Hakika yeye atasaidiwa (na sharia maadam anayo haki).

وَلَا تَقْرَبُوا مَالَ الْيَتِيمِ إِلَّا بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ حَتَّىٰ
يَبْلُغَ أَشُدَّهُ ۚ وَأَوْفُوا بِالْعَهْدِ ۖ إِنَّ الْعَهْدَ كَانَ
مَسْئُولًا ﴿٣٤﴾

34. Wala msiyakaribie (msiyaguse) mali ya yatima, isipokuwa kwa njia iliyo bora (kwa hao mayatima) mpaka afike baleghe yake (huyo yatima akabidhiwe mwenyewe). Na timizeni ahadi. Kwa hakika ahadi itaulizwa (Siku ya Kiama).

وَأَوْفُوا الْكَيْلَ إِذَا كِلْتُمْ وَزِنُوا بِالْقِسْطَاسِ
الْمُسْتَقِيمِ ۚ ذَٰلِكَ خَيْرٌ وَأَحْسَنُ تَأْوِيلًا ﴿٣٥﴾

35. Na timizeni kipimo mpimapo; na pimeni kwa mizani zilizo sawa. Hayo ni wema kwenu na bora mwishoni (kwake).

وَلَا تَقْفُ مَا لَيْسَ لَكَ بِهِ عِلْمٌ ۚ إِنَّ السَّمْعَ وَالْبَصَرَ
وَالْفُؤَادَ كُلُّ أُولَٰئِكَ كَانَ عَنْهُ مَسْئُولًا ﴿٣٦﴾

36. Wala usifuate (ukipita ukiyasema au kuyafanya) usiyo na ilimu (ujuzi) nayo. Hakika masikio na macho na moyo; hivyo vyote vitaulizwa.

وَلَا تَمْشِ فِي الْأَرْضِ مَرَحًا ۖ إِنَّكَ لَن تَخْرِقَ
الْأَرْضَ وَلَن تَبْلُغَ الْجِبَالَ طُولًا ﴿٣٧﴾

37. Wala usitembee (usende) katika ardhi kwa maringo. Hakika wewe huwezi kuipasua ardhi wala huwezi kufikia urefu wa milima. (Basi unajivuna nini).

كُلُّ ذَٰلِكَ كَانَ سَيِّئُهُ عِندَ رَبِّكَ مَكْرُوهًا ﴿٣٨﴾

38. Haya yote ubaya wake ni wenye kuchukiza mbele ya Mola wako.

ذَٰلِكَ مِمَّا أَوْحَىٰ إِلَيْكَ رَبُّكَ مِنَ الْحِكْمَةِ ۗ وَلَا تَجْعَلْ
مَعَ اللَّهِ إِلَٰهًا آخَرَ فَتُلْقَىٰ فِي جَهَنَّمَ مَلُومًا مَّدْحُورًا ﴿٣٩﴾

39. Haya ni katika yale aliyokufunulia Mola wako katika hikima (zake). Wala usimueke pamoja na Mwenyezi Mungu, mungu mwengine, usije kutupwa katika Jahanamu hali ya kuwa mwenye kulaumiwa (na) mwenye kufukuzwa (huku na huku).

أَفَأَصْفَاكُمْ رَبُّكُم بِالْبَنِينَ وَاتَّخَذَ مِنَ الْمَلَائِكَةِ
إِنَاثًا ۚ إِنَّكُمْ لَتَقُولُونَ قَوْلًا عَظِيمًا ﴿٤٠﴾ ع

40. Je! Mola wenu amekuchagulieni watoto wanaume, na Mwenyewe akajifanyia watoto wanawake katika Malaika? Kwa hakika nyinyi mnasema maneno makubwa (kabisa).

---

34. Imeshadidishwa sana adhabu ya anayemdhulumu yatima haki yake, bali asiyemtazama tu kwa rehema— seuze anayemdhulumu. Na kila mnyonge ndiyo vivi hivi. Lakini huyu yatima imezidi kwa vile ni mdogo na hana wa kumsimamia.

Basi natutahadhari kutomtazama yatima kwa jicho la rehema, akitukhusu asitukhusu.

Na tujitahidi kweli kweli kumlea kwa vizuri kama tunavyolea watoto wetu. Hili ni moja kubwa kabisa la kujivutia mtu mwenyewe— na watu wake — rehema ya dunia na Akhera.

| | |
|---|---|
| Ukilea mwana mwema | Na mwana mui mlele (mlee) |
| Mwema ukimpa chenga | Na mui mpe chelele (chenga ndogo) |
| Humjui mja kufaa | Mja-kupa maji mbele |

35. Mambo yameharibika kweli kweli. Wanaopima kwa vibaba na pishi wanaghushi! Wanaopima kwa magunia wanaghushi! KUGHUSHI WAMEBARIZI katika kila jambo.

40. Makafiri wa Kiarabu walikuwa wakiitakidi kuwa Malaika ni watoto wanawake wa Mwenyezi Mungu.

41. Na tumekwisha kueleza (kila jambo) katika hii Qurani (kwa namna namna) ili wapate kukumbuka; lakini haiwazidishii (hao wabaya) ila kuichukia (tu).

وَلَقَدْ صَرَّفْنَا فِيْ هٰذَا الْقُرْاٰنِ لِيَذَّكَّرُوْا ؕ وَمَا
يَزِيْدُهُمْ اِلَّا نُفُوْرًا ﴿۴۱﴾

42. Sema: "Lau wangalikuwa pamoja naye (Mwenyezi Mungu) waungu (wengine) kama wasemavyo, basi wangalitafuta njia ya kufikia kwa Mwenyezi Mungu (kupigana naye)."

قُلْ لَّوْ كَانَ مَعَهٗۤ اٰلِهَةٌ كَمَا يَقُوْلُوْنَ اِذًا لَّابْتَغَوْا
اِلٰى ذِى الْعَرْشِ سَبِيْلًا ﴿۴۲﴾

43. Ametakasika Mwenyezi Mungu na ameepukana, na hayo wasemayo, kwa uepukano mkubwa (kabisa).

سُبْحٰنَهٗ وَ تَعٰلٰى عَمَّا يَقُوْلُوْنَ عُلُوًّا كَبِيْرًا ﴿۴۳﴾

44. Zinamtukuza zote mbingu saba na ardhi na vilivyomo ndani yake. Na hakuna chochote ila kinamsabihi (Mwenyezi Mungu) kwa sifa Zake njema. Lakini nyinyi hamfahamu kusabihi (kutukuza) kwake. Hakika Yeye Mwenyezi Mungu ni Mpole (na) Mwingi wa kusamehe.

تُسَبِّحُ لَهُ السَّمٰوٰتُ السَّبْعُ وَالْاَرْضُ وَمَنْ فِيْهِنَّ ؕ
وَاِنْ مِّنْ شَیْءٍ اِلَّا يُسَبِّحُ بِحَمْدِهٖ وَلٰكِنْ لَّا تَفْقَهُوْنَ
تَسْبِيْحَهُمْ ؕ اِنَّهٗ كَانَ حَلِيْمًا غَفُوْرًا ﴿۴۴﴾

45. Na unaposoma Qurani (inakuwa kama kwamba) tumetia baina yako na baina ya wale wasioamini akhera pazia lililofunikwa (sana hata hawafahamu kinachosemwa)

وَاِذَا قَرَاْتَ الْقُرْاٰنَ جَعَلْنَا بَيْنَكَ وَبَيْنَ الَّذِيْنَ لَا
يُؤْمِنُوْنَ بِالْاٰخِرَةِ حِجَابًا مَّسْتُوْرًا ﴿۴۵﴾

46. Na (kama kwamba) tumetia vifuniko nyoyoni mwao wasije wakaifahamu na (kama tumetia) katika masikio yao uzito (uziwi). Na unapomtaja Mola wako katika Qurani peke yake, basi wao hugeuza migongo yao kwa kuchukia; (wanaona itamkinika vipi kuwa Mungu Mmoja).

وَّ جَعَلْنَا عَلٰى قُلُوْبِهِمْ اَكِنَّةً اَنْ يَّفْقَهُوْهُ وَفِيْۤ
اٰذَانِهِمْ وَقْرًا ؕ وَاِذَا ذَكَرْتَ رَبَّكَ فِى الْقُرْاٰنِ وَحْدَهٗ
وَلَّوْا عَلٰۤى اَدْبَارِهِمْ نُفُوْرًا ﴿۴۶﴾

47. Tunajua sana sababu wanayosikilizia, wanapokusikiliza, na wanaponong'ona; wanaposema hao madhalimu (kuwaambia Waislamu kwa ajili ya kutaka kuwapoteza); "Ninyi hamumfuati isipokuwa mtu aliyerogwa."

نَحْنُ اَعْلَمُ بِمَا يَسْتَمِعُوْنَ بِهٖۤ اِذْ يَسْتَمِعُوْنَ اِلَيْكَ
وَاِذْ هُمْ نَجْوٰۤى اِذْ يَقُوْلُ الظّٰلِمُوْنَ اِنْ تَتَّبِعُوْنَ اِلَّا
رَجُلًا مَّسْحُوْرًا ﴿۴۷﴾

48. Tazama jinsi wanavyokupigia mifano (ya uwongo; mara amerogwa, mara muongo, mara. . .). Basi wakapotea; kwa hivyo hawawezi kupata njia (ya kuwapelekea katika haki).

اُنْظُرْ كَيْفَ ضَرَبُوْا لَكَ الْاَمْثَالَ فَضَلُّوْا فَلَا
يَسْتَطِيْعُوْنَ سَبِيْلًا ﴿۴۸﴾

49. Na walisema: "Je! Tutakapokuwa mifupa na mapande yaliyosagikasagika tutafufuliwa kuwa viumbe wapya?

وَ قَالُوْۤا ءَاِذَا كُنَّا عِظَامًا وَّرُفَاتًا ءَاِنَّا
لَمَبْعُوْثُوْنَ خَلْقًا جَدِيْدًا ﴿۴۹﴾

50. Sema: "Kuweni mawe au chuma "

قُلْ كُوْنُوْا حِجَارَةً اَوْ حَدِيْدًا ﴿۵۰﴾

---

47. Sababu yake ni kuwa wanatafuta njia ya kuwapoteza Waislamu na wanakuja kusikiliza ili wakazuwe.

49-51. Ati wanaona kuwa Mwenyezi Mungu hana uweza wa kumfufua mwanadamu. Ndiyo wanaambiwa "Nawawe na nguvu hata za kiumbe gani hicho chenye nguvu kuliko chochote," na wakifa, Mwenyezi Mungu anaweza kuwafufua.

51. "Au kiumbe chochote katika vile vinavyoonekana vigumu katika nyoyo (fikra) zenu. (Basi hata mkiwa hivyo mtafufuliwa.)" Hapo Watasema: "Ni nani atakayeturudisha (hivyo)?" Sema: "Ni yule aliyekuumbeni mara ya kwanza." Hapo watakutikisia vichwa vyao na watasema: "Yatakuwa lini hayo?" Sema: "Huwenda yakawa karibu."

أَوْ خَلْقًا مِّمَّا يَكْبُرُ فِي صُدُورِكُمْ ۚ فَسَيَقُولُونَ مَن يُعِيدُنَا ۖ قُلِ الَّذِي فَطَرَكُمْ أَوَّلَ مَرَّةٍ ۚ فَسَيُنْغِضُونَ إِلَيْكَ رُءُوسَهُمْ وَيَقُولُونَ مَتَىٰ هُوَ ۖ قُلْ عَسَىٰ أَن يَكُونَ قَرِيبًا ﴿٥١﴾

52. "(Yatakuwa) siku atakapokwiteni (Mwenyezi Mungu), na nyinyi mtaitika kwa kumshukuru, na mtafahamu kuwa hamkukaa (duniani) ila muda mdogo tu."

يَوْمَ يَدْعُوكُمْ فَتَسْتَجِيبُونَ بِحَمْدِهِ وَتَظُنُّونَ إِن لَّبِثْتُمْ إِلَّا قَلِيلًا ﴿٥٢﴾

53. Na waambie waja wangu waseme (daima maneno) yaliyo mazuri; maana Shetani huchochea (ugomvi) baina yao. Hakika Shetani kwa mwanadamu ni adui aliye dhahiri.

وَقُل لِّعِبَادِي يَقُولُوا الَّتِي هِيَ أَحْسَنُ ۚ إِنَّ الشَّيْطَانَ يَنزَغُ بَيْنَهُمْ ۚ إِنَّ الشَّيْطَانَ كَانَ لِلْإِنسَانِ عَدُوًّا مُّبِينًا ﴿٥٣﴾

54. Mola wenu anakujueni sana. Akipenda atakurehemuni (maadamu mtatubia kwake), na akipenda atakuadhibuni (maadamu mtaendelea na maasiya yenu). Na hatukukutuma (hatukukuleta) kuwa mlinzi juu yao; (tumekuleta uwe Mtume tu).

رَّبُّكُمْ أَعْلَمُ بِكُمْ ۖ إِن يَشَأْ يَرْحَمْكُمْ أَوْ إِن يَشَأْ يُعَذِّبْكُمْ ۚ وَمَا أَرْسَلْنَاكَ عَلَيْهِمْ وَكِيلًا ﴿٥٤﴾

55. Na Mola wako anawajua sana wote waliomo katika mbingu na ardhi. Na kwa hakika tuliwafadhilisha baadhi ya Manabii kuliko wengine (kwa amali zao zilizo bora zaidi kuliko za wenziwao); na Daudi tulimpa Zaburi.

وَرَبُّكَ أَعْلَمُ بِمَن فِي السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ ۗ وَلَقَدْ فَضَّلْنَا بَعْضَ النَّبِيِّينَ عَلَىٰ بَعْضٍ ۖ وَآتَيْنَا دَاوُودَ زَبُورًا ﴿٥٥﴾

56. Sema: "Waiteni wale mnaodai (kuwa ni waungu) mkamwacha Yeye (ili wakuondosheeni baa zinazokufikieni). Hawataweza kukuondosheeni shari wala kubadilisha (kuwa kheri)."

قُلِ ادْعُوا الَّذِينَ زَعَمْتُم مِّن دُونِهِ فَلَا يَمْلِكُونَ كَشْفَ الضُّرِّ عَنكُمْ وَلَا تَحْوِيلًا ﴿٥٦﴾

57. Hao wanaowaomba, (wenyewe) wanatafuta ukaribiano na Mola wao; (hata) walio karibu sana miongoni mwao (na Mungu, kama Malaika, wao wanafanya yaya haya) wanatumai rehema zake na

أُولَٰئِكَ الَّذِينَ يَدْعُونَ يَبْتَغُونَ إِلَىٰ رَبِّهِمُ الْوَسِيلَةَ أَيُّهُمْ أَقْرَبُ وَيَرْجُونَ رَحْمَتَهُ وَيَخَافُونَ

---

53. Kupandana maneno ndiyo asili ya gomvi zote kubwa—zikiwa za nyumbani au za nje au za madola pia. Basi natutahadhari na kupandisha maneno. Mwenzako—mkeo au mumeo au mwengine yoyote yule—kikipanda kiungulia chake au umempanda wazimu wake, au kimemjia kidudu chake, akawa anafoka; wewe jinyamzie kimya hata akikutukana vipi; uone kuwa "Leo ni siku yake" Na ukiona atazidi ondoka. Na siku yako naye akufanyie hivi. Mkenda mwendo huu shetani atarudi—ataruka—pa tupu.

54. Wala si ovyo ovyo kama tulivyobainisha mara nyingi—kwa kufuata alivyosema Mwenyewe Mwenyezi Mungu na Mtumewe. Lakini anayestahiki kurehemewa humrehemu na anayestahiki kuadhibiwa humuadhibu ikiwa kapindukia sana mipaka au humsamehe ikiwa hakupindukia mipaka.

55. Ndiyo hayo hayo yanayosemwa kila wakati: kila watu wanalipwa kwa amali wanazozifanya—mema kwa mema na mabaya kwa mabaya. Na watu wanazidiana katika huo wema na huo ubaya. Basi kila anayezidi katika huo wema anakuwa bora zaidi kuliko hao aliowazidi. Basi hao Mitume wamezidiana katika kazi zao za wema. Na wabaya vile vile wanazidiana.

57. Yaani hao wanaowaabudu—kama hao Malaika na Nabii Isa—wenyewe nafsi zao wanamuabudu Mwenyezi Mungu.

عَذَابَهُ ۚ إِنَّ عَذَابَ رَبِّكَ كَانَ مَحْذُورًا ﴿٥٧﴾

wanaogopa adhabu Yake. Hakika adhabu ya Mola wako ni ya kuogopwa.

وَإِن مِّن قَرْيَةٍ إِلَّا نَحْنُ مُهْلِكُوهَا قَبْلَ يَوْمِ الْقِيَامَةِ
أَوْ مُعَذِّبُوهَا عَذَابًا شَدِيدًا ۚ كَانَ ذَٰلِكَ فِي الْكِتَابِ
مَسْطُورًا ﴿٥٨﴾

58. Na hakutakuwa mji wowote ila Sisi tutauhilikisha kabla ya siku ya Kiama au tutauadhibu adhabu kali (kama unastahiki hayo). Haya yameandikwa katika Kitabu (kilichoandika kila kitu).

وَمَا مَنَعَنَا أَن نُّرْسِلَ بِالْآيَاتِ إِلَّا أَن كَذَّبَ بِهَا
الْأَوَّلُونَ ۚ وَآتَيْنَا ثَمُودَ النَّاقَةَ مُبْصِرَةً فَظَلَمُوا بِهَا ۚ
وَمَا نُرْسِلُ بِالْآيَاتِ إِلَّا تَخْوِيفًا ﴿٥٩﴾

59. Na hakuna kinachotuzuia kuileta miujiza (waitakayo) ila ni kuwa watu wa zamani waliikadhibisha. Na tuliwapa Wathamudi ngamia jike kuwa Ishara iliyo dhahiri (muujiza), lakini wakamkanusha. Na hatuzipeleki hizo ishara ila kwa ajili ya kuhadharisha. (Na hawatahadhari).

وَإِذْ قُلْنَا لَكَ إِنَّ رَبَّكَ أَحَاطَ بِالنَّاسِ ۚ وَمَا جَعَلْنَا
الرُّؤْيَا الَّتِي أَرَيْنَاكَ إِلَّا فِتْنَةً لِّلنَّاسِ وَالشَّجَرَةَ
الْمَلْعُونَةَ فِي الْقُرْآنِ ۚ وَنُخَوِّفُهُمْ فَمَا يَزِيدُهُمْ
ع إِلَّا طُغْيَانًا كَبِيرًا ﴿٦٠﴾

60. Na (kumbuka) tulipokwambia: "Hakika Mola wako amekwisha wazunguka hao watu (wabaya; atawatia mkononi. Na kweli akawatia mkononi). Na hatukuifanya ndoto ile tuliyokuonyesha ila kuwajaribu watu (wataamini au hawataamini). (Na kutajwa) katika Qurani (ule) mti uliolaaniwa (ni mtihani pia). Na tunawahadharisha lakini hayawazidishii (mahadhirisho yetu) ila uasi tu mkubwa.

وَإِذْ قُلْنَا لِلْمَلَائِكَةِ اسْجُدُوا لِآدَمَ فَسَجَدُوا إِلَّا
إِبْلِيسَ قَالَ أَأَسْجُدُ لِمَنْ خَلَقْتَ طِينًا ﴿٦١﴾

61. Na (kumbusha) tulipowaambia Malaika: "Msujudieni Adamu." Wakamsujudia isipokuwa Ibilisi. Akasema: "Je! Nimsujudie yule uliyemuumba kwa udongo."

قَالَ أَرَأَيْتَكَ هَٰذَا الَّذِي كَرَّمْتَ عَلَيَّ لَئِنْ أَخَّرْتَنِ
إِلَىٰ يَوْمِ الْقِيَامَةِ لَأَحْتَنِكَنَّ ذُرِّيَّتَهُ إِلَّا قَلِيلًا ﴿٦٢﴾

62. Akasema (tena kumwambia Mwenyezi Mungu): "Unaona! Huyu uliyempa Hishima zaidi kuliko mimi. Kama ukinipa muda mpaka siku ya Kiama, bila shaka nitakiangamiza kizazi chake (chote) ila wachache tu."

قَالَ اذْهَبْ فَمَن تَبِعَكَ مِنْهُمْ فَإِنَّ جَهَنَّمَ جَزَاؤُكُمْ
جَزَاءً مَّوْفُورًا ﴿٦٣﴾

63. (Mwenyezi Mungu) akasema: "Ondoka! (Ondokelea mbali)! Atakayekufuata miongoni mwao, basi hakika Jahanamu ndiyo malipo yenu, malipo kamili."

وَاسْتَفْزِزْ مَنِ اسْتَطَعْتَ مِنْهُم بِصَوْتِكَ وَأَجْلِبْ
عَلَيْهِم بِخَيْلِكَ وَرَجِلِكَ وَشَارِكْهُمْ فِي الْأَمْوَالِ
وَالْأَوْلَادِ وَعِدْهُمْ ۚ وَمَا يَعِدُهُمُ الشَّيْطَانُ إِلَّا غُرُورًا ﴿٦٤﴾

64. "Na wavute uwawezao miongoni mwao kwa sauti yako, na uwakusanyie (jeshi lako la) wapandao farasi na waendao kwa miguu. Na shirikiana nao katika mali (yao) na watoto (wao), na waahidi (ahadi za uwongo). Lakini Shetani hawapi waadi ila wa udanganyifu (kwani hana lake jambo).

---

60. Khabari za Miraji ni kama huo Mti uliolaaniwa na kama huo mti wa Mzagumi (mti mchungu kabisa) utakaokuwapo Motoni na mti wa Dharii (wenye miba mingi na mikali mno).

61. Wametia hapa ule uwongo walioutia katika ile Aya yake waliyoifanya kuwa ni ya 2.

61-70. Wamesimangwa kwa wizi wao wa fadhila na namna gani Mwenyezi Mungu alivyowafadhilisha juu ya viumbe vingi kabisa, na wao hawashukuru.

64. Wapandao farasi au wendao kwa miguu, muradi wake kuwatafutia kila njia za kuwapoteza, hutaweza kuwapoteza ila wale watakaotaka wenyewe kupotea. Siyo wewe una Nguvu (Power) za kuwapoteza.

65. "Hakika waja wangu huna mamlaka juu yao. Na Mola wako anatosha kuwa Mlinzi (wao)."

إِنَّ عِبَادِي لَيْسَ لَكَ عَلَيْهِمْ سُلْطَانٌ ۚ وَكَفَىٰ بِرَبِّكَ وَكِيلًا ﴿٦٥﴾

66. Mola wenu ni yule anayekuendesheeni marikebu katika bahari ili mtafute fadhila (riziki) Zake. Bila shaka Yeye ni Mwingi wa rehemu kwenu.

رَبُّكُمُ الَّذِي يُزْجِي لَكُمُ الْفُلْكَ فِي الْبَحْرِ لِتَبْتَغُوا مِنْ فَضْلِهِ ۚ إِنَّهُ كَانَ بِكُمْ رَحِيمًا ﴿٦٦﴾

67. Na inapokufikieni taabu katika bahari, hupotea wale mnaowaita (waungu, hamuwataji) isipokuwa Yeye tu (Mungu wa haki). Lakini anapokufikisheni salama nchi kavu, mnakengeuka. Ama mwanaadamu ni mwingi wa kukanusha (neema za Mwenyezi Mungu).

وَإِذَا مَسَّكُمُ الضُّرُّ فِي الْبَحْرِ ضَلَّ مَنْ تَدْعُونَ إِلَّا إِيَّاهُ ۖ فَلَمَّا نَجَّاكُمْ إِلَى الْبَرِّ أَعْرَضْتُمْ ۚ وَكَانَ الْإِنْسَانُ كَفُورًا ﴿٦٧﴾

68. Je! Mumeaminisha ya kuwa (Mungu hatakudidimizeni upande wowote wa nchi kavu au hatakuleteeni tufani ya mchanga (au mawe), kisha msipate mlinzi (wa kukutengeni na hiyo adhabu ya Mwenyezi Mungu)?

أَفَأَمِنْتُمْ أَنْ يَخْسِفَ بِكُمْ جَانِبَ الْبَرِّ أَوْ يُرْسِلَ عَلَيْكُمْ حَاصِبًا ثُمَّ لَا تَجِدُوا لَكُمْ وَكِيلًا ﴿٦٨﴾

69. Au mumeaminisha ya kuwa hatakurudisheni humo (baharini) mara ya pili na kukuleteeni upepo mkali, akakuzamisheni, kwa sababu mumekufuru? Kisha hamtapata mwenye kukuteteeni (kukupiganieni) juu Yetu kwa (adhabu) hii.

أَمْ أَمِنْتُمْ أَنْ يُعِيدَكُمْ فِيهِ تَارَةً أُخْرَىٰ فَيُرْسِلَ عَلَيْكُمْ قَاصِفًا مِنَ الرِّيحِ فَيُغْرِقَكُمْ بِمَا كَفَرْتُمْ ۙ ثُمَّ لَا تَجِدُوا لَكُمْ عَلَيْنَا بِهِ تَبِيعًا ﴿٦٩﴾

70. Na hakika tumewatukuza wanaadamu na tumewapa vya kupanda barani na baharini, na tumewaruzuku vitu vizuri vizuri, na tumewatukuza kuliko wengi katika wale tuliowaumba, kwa utukufu ulio mkubwa (kabisa).

وَلَقَدْ كَرَّمْنَا بَنِي آدَمَ وَحَمَلْنَاهُمْ فِي الْبَرِّ وَالْبَحْرِ وَرَزَقْنَاهُمْ مِنَ الطَّيِّبَاتِ وَفَضَّلْنَاهُمْ عَلَىٰ كَثِيرٍ مِمَّنْ خَلَقْنَا تَفْضِيلًا ﴿٧٠﴾

71. (Wakumbushe) siku tutakapoweta kila watu pamoja na waongozi wao. Basi watakaopewa daftari zao kwa mikono ya kulia hao watasoma daftari zao (kwa furaha) wala hawatadhulumiwa kijijuzi kilichomo katika mpasuko wa kokwa ya tende; (yaani hawatadhulumiwa hata kitu kidogo).

يَوْمَ نَدْعُو كُلَّ أُنَاسٍ بِإِمَامِهِمْ ۖ فَمَنْ أُوتِيَ كِتَابَهُ بِيَمِينِهِ فَأُولَٰئِكَ يَقْرَءُونَ كِتَابَهُمْ وَلَا يُظْلَمُونَ فَتِيلًا ﴿٧١﴾

72. Na aliye kipofu katika hii, (dunia) basi atakuwa kipofu katika Akhera, na (atakuwa) aliyepotea zaidi njia (huko).

وَمَنْ كَانَ فِي هَٰذِهِ أَعْمَىٰ فَهُوَ فِي الْآخِرَةِ أَعْمَىٰ وَأَضَلُّ سَبِيلًا ﴿٧٢﴾

73. Na hakika walikuwa karibu kukukengeusha na yale tuliyofunulia (tuliyokuletea Wahyi) ili upate kutuzulia badala ya haya (ya haki tuliyokuteremshia); na hapo bila shaka wangalikufanya rafiki (yao mkubwa).

وَإِنْ كَادُوا لَيَفْتِنُونَكَ عَنِ الَّذِي أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ لِتَفْتَرِيَ عَلَيْنَا غَيْرَهُ ۖ وَإِذًا لَاتَّخَذُوكَ خَلِيلًا ﴿٧٣﴾

---

73-77. Walikuwa makafiri wakimtaka Mtume mara awafanyie hivi na mara awafanyie hivi, ndipo wamfuate. Katika waliyomwambia ni kama haya:– (a) Abudu waungu wetu mwaka mmoja pamoja na sisi; na tuabudu Mungu wako mwaka mmoja pamoja na wewe. Na hivi hivi maisha.
(b) Tuondoshee kufurama katika sala, ndio tutakufuata (Ati waondoshewe kurukuu na kusujudu).
(c) Tuondoshee kutoa zaka na masadaka. (d) Nenda kakae Shamu, kama Mitume wengine, ndiyo tukufuate. Na kama haya.

74. Na kama tusingalikuthibitisha ungalikuwa karibu kuwaelekea kidogo

وَلَوْلَآ أَنْ ثَبَّتْنٰكَ لَقَدْ كِدْتَّ تَرْكَنُ إِلَيْهِمْ شَيْـًٔا قَلِيْلًا ﴿٧٤﴾

75. Hapo bila shaka tungalikuonjesha adhabu kubwa ya maisha (ya hapa Ulimwenguni na adhabu kubwa ya maisha ya akhera;) kisha usingepata msaidizi wa kukunusuru juu yetu.

إِذًا لَّأَذَقْنٰكَ ضِعْفَ الْحَيٰوةِ وَضِعْفَ الْمَمَاتِ ثُمَّ لَا تَجِدُ لَكَ عَلَيْنَا نَصِيْرًا ﴿٧٥﴾

76. Na kwa hakika walikaribia kukufukuza katika nchi (hii ya Madina) ili wakutoe humo. Na wasingalikaa baada yako ila (muda) mchache tu. (Tungewaagamiza).

وَإِنْ كَادُوْا لَيَسْتَفِزُّوْنَكَ مِنَ الْأَرْضِ لِيُخْرِجُوْكَ مِنْهَا وَإِذًا لَّا يَلْبَثُوْنَ خِلٰفَكَ إِلَّا قَلِيْلًا ﴿٧٦﴾

77. Ndiyo desturi ya wale tuliowatuma (tuliowapa Utume) kabla yako katika Mitume wetu. Wala hutapata mabadiliko katika desturi Yetu.

سُنَّةَ مَنْ قَدْ أَرْسَلْنَا قَبْلَكَ مِنْ رُّسُلِنَا وَلَا تَجِدُ لِسُنَّتِنَا تَحْوِيْلًا ﴿٧٧﴾ ع

78. Simamisha Sala jua linapopinduka (likenda magharibi) mpaka giza la usiku; na (msiache) Qurani ya (sala ya) alfajiri. Hakika (kusoma) Qurani katika (kusali Sala ya) alfajiri kunahudhuriwa (na Malaika).

أَقِمِ الصَّلٰوةَ لِدُلُوْكِ الشَّمْسِ إِلٰى غَسَقِ الَّيْلِ وَقُرْاٰنَ الْفَجْرِ إِنَّ قُرْاٰنَ الْفَجْرِ كَانَ مَشْهُوْدًا ﴿٧٨﴾

79. Na katika usiku jiondoshee usingizi (kidogo) kwa (kusoma) hiyo (Qurani ndani ya Sala). Hiyo ni (ibada) zaidi kwako. Huwenda Mola wako akakuinua cheo kinachosifika.

وَمِنَ الَّيْلِ فَتَهَجَّدْ بِهٖ نَافِلَةً لَّكَ عَسٰٓى أَنْ يَّبْعَثَكَ رَبُّكَ مَقَامًا مَّحْمُوْدًا ﴿٧٩﴾

80. Na sema (katika kuomba dua kwako): "Mola wangu! Niingize mwingizo mwema, na nitoe kutoka kwema. Na unipe nguvu zinazotoka kwako zinazosaidia."

وَقُلْ رَّبِّ أَدْخِلْنِيْ مُدْخَلَ صِدْقٍ وَّأَخْرِجْنِيْ مُخْرَجَ صِدْقٍ وَّاجْعَلْ لِّيْ مِنْ لَّدُنْكَ سُلْطٰنًا نَّصِيْرًا ﴿٨٠﴾

81. Na sema: "Ukweli umefika; na uwongo umetoweka (umekwishaondoka). Uwongo (mwishowe) huwa ndio wenye kutoweka (kuondoka)."

وَقُلْ جَآءَ الْحَقُّ وَزَهَقَ الْبَاطِلُ إِنَّ الْبَاطِلَ كَانَ زَهُوْقًا ﴿٨١﴾

82. Na tunateremsha katika Qurani (hayo mafundisho yake) ambayo ni ponyo (poza la nyoyo) na rehema kwa wanaoamini. Wala hayawazidishi

وَنُنَزِّلُ مِنَ الْقُرْاٰنِ مَا هُوَ شِفَآءٌ وَّرَحْمَةٌ

---

78. Nusu nzima ya mwanzo ya mchana halazimishwi mtu kusali mpaka jua linapopinduka kwenda upande wa magharibi ndipo anapoambiwa Asali Sala ya Adhuhuri. Hata baada ya saa 3 hivi ndipo anapoambiwa asali Sala ya Laasiri. Hata baada ya saa 3 hivi ndipo anapoambiwa asali Sala ya Magharibi. Hata baada ya saa unusu hivi ndipo anapoambiwa asali Sala ya Isha. Kisha anaachiwa usiku kucha (halazimishwi kusali) mpaka Alfajiri; asali Sala ya Asubuhi (ya Alfajiri).

Na hapana Sala bora zaidi kuliko hiyo Sala ya Alfajiri, na hapana Sala ngumu zaidi kuliko hii pia.

79. Kusali mtu mwenyewe usiku Sala azitakazo ni Suna Kubwa, Lakini si wajibu. Na inataka Mwislamu awe anasali usiku nyumbani kwake japokuwa Rakaa tatu za Witr au rakaa moja pia.

82. Hayo ni baadhi ya neema zilizopatikana kwa kuteremka Qurani. Poza lililotajwa ni poza la nyoyo. Qurani siyo kazi yake kuponesha Madonda wala Matumbo wala Mishipa wala Vifua Vikuu wala Vidogo wala magonjwa mengine. Mwenyewe Mtume akiwaamrisha Masahaba zake wende kwa madaktari wakafanye dawa; bali hata madaktari waliokuwa makafiri. Mtume alimuamrisha Sahaba mkubwa, Bwana Saad bin Abi Waqqas—walipokwenda Makka kuhiji akazidiwa na ugonjwa. Mtume alimwambia afunge safari ya kiasi cha meli 70 ende Taif kumfuatia daktari wa kikafiri aliyekuwako huko—Harith bin Kalada.

(mafundisho haya) madhalimu ila khasara tu (kwani hawakubali kuyafuata).

لِلْمُؤْمِنِينَ ۙ وَلَا يَزِيدُ الظَّالِمِينَ إِلَّا خَسَارًا ﴿٨٢﴾

83. Na tunapomneemesha mwanaadamu, hukengeuka na kujitenga upande (na amri zetu). Na inapomgusa shari mara hukata tamaa (akawa katika unyenyekevu mkubwa).

وَإِذَا أَنْعَمْنَا عَلَى الْإِنْسَانِ أَعْرَضَ وَنَأَىٰ بِجَانِبِهِ ۖ
وَإِذَا مَسَّهُ الشَّرُّ كَانَ يَئُوسًا ﴿٨٣﴾

84. Sema: "Kila mmoja anafanya (amali zake) kwa njia yake. Na Mola wetu anajua aliyeongoka katika njia (wanazofuata)."

قُلْ كُلٌّ يَعْمَلُ عَلَىٰ شَاكِلَتِهِ فَرَبُّكُمْ أَعْلَمُ بِمَنْ
هُوَ أَهْدَىٰ سَبِيلًا ﴿٨٤﴾

85. Na wanakuuliza habari ya roho. Sema: "Roho ni jambo lililokhusika na Mola wangu (Mwenyezi Mungu). Nanyi hamkupewa katika ilimu (ujuzi) ila kidogo kabisa. (Nayo ni ilimu ya vitu visivyokhusika na roho)."

وَيَسْأَلُونَكَ عَنِ الرُّوحِ ۖ قُلِ الرُّوحُ مِنْ أَمْرِ رَبِّي
وَمَا أُوتِيتُمْ مِنَ الْعِلْمِ إِلَّا قَلِيلًا ﴿٨٥﴾

86. Na kama tungelipenda bila shaka tungaliondoa yale tuliyokufunulia, kisha usingalipata kwa (jambo) hili wa kukupigania juu Yetu.

وَلَئِنْ شِئْنَا لَنَذْهَبَنَّ بِالَّذِي أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ ثُمَّ لَا
تَجِدُ لَكَ بِهِ عَلَيْنَا وَكِيلًا ﴿٨٦﴾

87. Ila kwa rehema itokayo kwa Mola wako (ndio yakakudumia haya). Hakika fadhila Yake (Mwenyezi Mungu) iliyo juu yako ni kubwa kabisa.

إِلَّا رَحْمَةً مِنْ رَبِّكَ ۚ إِنَّ فَضْلَهُ كَانَ عَلَيْكَ
كَبِيرًا ﴿٨٧﴾

88. Sema "Hata wakijikusanya watu (wote) na majinni ili kuleta mfano wa hii Qurani basi hawangaliweza kuleta mfano wake; hata kama watasaidiana (vipi) wao kwa wao."

قُلْ لَئِنِ اجْتَمَعَتِ الْإِنْسُ وَالْجِنُّ عَلَىٰ أَنْ يَأْتُوا
بِمِثْلِ هَٰذَا الْقُرْآنِ لَا يَأْتُونَ بِمِثْلِهِ وَلَوْ كَانَ
بَعْضُهُمْ لِبَعْضٍ ظَهِيرًا ﴿٨٨﴾

89. Na bila shaka tumewaeleza watu kwa namna nyingi katika hii Qurani kila mfano. Lakini watu wengi wanakataa (kila kitu) isipokuwa kukanusha tu.

وَلَقَدْ صَرَّفْنَا لِلنَّاسِ فِي هَٰذَا الْقُرْآنِ مِنْ كُلِّ
مَثَلٍ فَأَبَىٰ أَكْثَرُ النَّاسِ إِلَّا كُفُورًا ﴿٨٩﴾

90. Na walisema (makafiri wa Kiqureshi kumwambia Mtume): "Hatuwezi kukuamini mpaka utububujishie (utupitishie) chemchemu katika ardhi (hii yetu ya Makka)"

وَقَالُوا لَنْ نُؤْمِنَ لَكَ حَتَّىٰ تَفْجُرَ لَنَا مِنَ الْأَرْضِ
يَنْبُوعًا ﴿٩٠﴾

91. "Au uwe na bustani ya mitende na mizabibu; kisha ububujishe (upitishe) mito katikati yake kwa mabubujiko makubwa"

أَوْ تَكُونَ لَكَ جَنَّةٌ مِنْ نَخِيلٍ وَعِنَبٍ فَتُفَجِّرَ
الْأَنْهَارَ خِلَالَهَا تَفْجِيرًا ﴿٩١﴾

92. "Au utuangushie mbingu vipande vipande kama ulivyodai, au utuletee Mwenyezi Mungu na Malaika uso kwa uso"

أَوْ تُسْقِطَ السَّمَاءَ كَمَا زَعَمْتَ عَلَيْنَا كِسَفًا أَوْ
تَأْتِيَ بِاللَّهِ وَالْمَلَائِكَةِ قَبِيلًا ﴿٩٢﴾

---

84. Haya ndiyo yale yale ya kusema kuwa mtu amepewa nguvu (power) za kufanya mema na mabaya, kama tulivyobainisha katika Aya ya 35 ya *Suratun Nahl.*

88. Mtihani huu wamepewa katika Sura nyingi. Nao kabisa hawakuweza kuufanya. Wala hakuna kiumbe chochote kitakachoweza kuufanya.

90-93. Katika hivyo vituko vyao walivyokuwa wakitaka kumshindia Mtume.

93. "Au uwe na nyumba ya dhahabu, au upande mbinguni. Na hatutaamini kupanda kwako mpaka ututeremshie kitabu tukisome." (Mungu anamwambia Mtume) Sema: "Subhanallah! (Mola wangu ni Mtakatifu!). Mimi sikuwa ila ni mtu (tu, niliyefanywa) Mtume." 'Si Malaika wala si Mungu. (Nitafanya vipi hayo?)

أَوْ يَكُونَ لَكَ بَيْتٌ مِّن زُخْرُفٍ أَوْ تَرْقَىٰ
فِي السَّمَاءِ ۖ وَلَن نُّؤْمِنَ لِرُقِيِّكَ حَتَّىٰ تُنَزِّلَ عَلَيْنَا
كِتَابًا نَّقْرَؤُهُ ۗ قُلْ سُبْحَانَ رَبِّي هَلْ كُنتُ إِلَّا بَشَرًا
رَّسُولًا ﴿٩٣﴾

94. Na hapana lililowazuilia watu kuamini ulipowajia uwongofu isipokuwa walisema. "Je! Mwenyezi Mungu humtuma binadamu kuwa mjumbe (wake)?"

وَمَا مَنَعَ النَّاسَ أَن يُؤْمِنُوا إِذْ جَاءَهُمُ الْهُدَىٰ
إِلَّا أَن قَالُوا أَبَعَثَ اللَّهُ بَشَرًا رَّسُولًا ﴿٩٤﴾

95. Sema: "Kama katika ardhi wangalikuwa Malaika (wanaokuwako papa hapa,) wanakwenda (na kurejea), wametua (maskanini mwao; majumbani mwao hapa ardhini), bila shaka tungaliwateremshia kutoka mbinguni Malaika kuwa Mtume wao.(Lakini maadamu wako binadamu, mwenzao atakuwa Mtume wao)."

قُل لَّوْ كَانَ فِي الْأَرْضِ مَلَائِكَةٌ يَمْشُونَ
مُطْمَئِنِّينَ لَنَزَّلْنَا عَلَيْهِم مِّنَ السَّمَاءِ مَلَكًا رَّسُولًا ﴿٩٥﴾

96. Sema: "Mwenyezi Mungu anatosha kuwa Shahidi baina yangu na baina yenu (kuwa mimi ni Mtume wake). Hakika Yeye anawajua vyema waja wake na anawaona."

قُلْ كَفَىٰ بِاللَّهِ شَهِيدًا بَيْنِي وَبَيْنَكُمْ ۚ إِنَّهُ
كَانَ بِعِبَادِهِ خَبِيرًا بَصِيرًا ﴿٩٦﴾

97. Na ambaye Mwenyezi Mungu anamwongoa, basi yeye ndiye aliyeongoka; na anawaachia kupotea, basi wewe hutawapatia walinzi wasiokuwa Yeye (Mwenyezi Mungu). Na tutawakusanya siku ya Kiama, hali kuwa wanakokotwa juu ya nyuso zao, na hali ya kuwa mapofu na mabubu na viziwi. Makazi yao ni Jahannamu. (Na) kila ukifanya kusinzia kidogo tutawazidishia mwako.

وَمَن يَهْدِ اللَّهُ فَهُوَ الْمُهْتَدِ ۖ وَمَن يُضْلِلْ فَلَن
تَجِدَ لَهُمْ أَوْلِيَاءَ مِن دُونِهِ ۖ وَنَحْشُرُهُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ
عَلَىٰ وُجُوهِهِمْ عُمْيًا وَبُكْمًا وَصُمًّا ۖ مَّأْوَاهُمْ جَهَنَّمُ ۖ
كُلَّمَا خَبَتْ زِدْنَاهُمْ سَعِيرًا ﴿٩٧﴾

98. Hayo ni malipo yao kwa sababu walizikanusha hoja zetu na wakasema: "Je! Tutakapokuwa mifupa na mapande yaliyosagika tutafufuliwa kuwa viumbe wapya?"

ذَٰلِكَ جَزَاؤُهُم بِأَنَّهُمْ كَفَرُوا بِآيَاتِنَا وَقَالُوا أَإِذَا كُنَّا
عِظَامًا وَرُفَاتًا أَإِنَّا لَمَبْعُوثُونَ خَلْقًا جَدِيدًا ﴿٩٨﴾

99. (Mwenyezi Mungu anasema): "Je! Hawakuona ya kwamba Mwenyezi Mungu aliyeziumba mbingu na ardhi ni Mwenye uweza wa kuumba mfano wa wao?" Na amewawekea muda usio na shaka (wa kuwafufua na kuwalipa). Lakini madhalimu wamekataa (kila kitu) isipokuwa kuendelea na ukafiri (wao).

أَوَلَمْ يَرَوْا أَنَّ اللَّهَ الَّذِي خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ
قَادِرٌ عَلَىٰ أَن يَخْلُقَ مِثْلَهُمْ وَجَعَلَ لَهُمْ أَجَلًا لَّا
رَيْبَ فِيهِ فَأَبَى الظَّالِمُونَ إِلَّا كُفُورًا ﴿٩٩﴾

---

93. Wamepindua makusudi maelezo ya Aya hii, wakasema kuwa hayo wameyataka makafiri waliposikia kuwa Mtume amekwenda Miiraji; na hali ya kuwa ni uwongo. Haya waliyataka makafiri siku za mwanzo za Uislamu wakati uliposhitadi ushindani. Lakini wao wamepachikia hivyo makusudi ili wakatae Miiraji na Israi, kama walivyofanya katika Sura nzima hii. Basi yote haya ni uwongo tu.

95. Wanapewa jawabu ya haki barabara. Lakini wapi wanasikia!

97. Tumetaja haya katika Aya ya 125 ya *Suratul An-Am.*

100. Sema: "Kama mngalizimiliki khazina za rehema ya Mola wangu, bila shaka mngalizuia kwa kuogopa kuzitumia (zisije zikesha). Na mwanaadamu ni choyo sana."

قُلْ لَّوْ اَنْتُمْ تَمْلِكُوْنَ خَزَآئِنَ رَحْمَةِ رَبِّيْٓ اِذًا لَّاَمْسَكْتُمْ
خَشْيَةَ الْاِنْفَاقِ ؕ وَكَانَ الْاِنْسَانُ قَتُوْرًا ﴿١٠٠﴾ ع

101. Na kwa yakini tulimpa Musa Hoja tisa zilizo wazi (za kuonyesha ukweli wa Utume wake). Waulize wana wa Israili alipowajia, na Firauni akamwambia: "Hakika mimi nakuona wewe Musa, umerogwa (umeharibika akili)."

وَلَقَدْ اٰتَيْنَا مُوْسٰى تِسْعَ اٰيٰتٍۢ بَيِّنٰتٍ فَسْــَٔلْ بَنِيْٓ اِسْرَآءِيْلَ
اِذْ جَآءَهُمْ فَقَالَ لَهٗ فِرْعَوْنُ اِنِّيْ لَاَظُنُّكَ يٰمُوْسٰى
مَسْحُوْرًا ﴿١٠١﴾

102. Akasema (Musa): "Bila shaka umekwishajua kuwa hakuna aliyeteremsha (Hoja) hizi isipokuwa Mola wa mbingu na ardhi, kuwa dalili; (ila unajibabaisha tu). Na hakika mimi nakuona, wewe Firauni, umekwishaangamia."

قَالَ لَقَدْ عَلِمْتَ مَآ اَنْزَلَ هٰٓؤُلَآءِ اِلَّا رَبُّ السَّمٰوٰتِ
وَالْاَرْضِ بَصَآئِرَ ۚ وَاِنِّيْ لَاَظُنُّكَ يٰفِرْعَوْنُ مَثْبُوْرًا ﴿١٠٢﴾

103. Basi (Firauni) akataka kuwafukuza katika nchi; kwa hivyo tukamzamisha yeye na waliokuwa pamoja naye wote

فَاَرَادَ اَنْ يَّسْتَفِزَّهُمْ مِّنَ الْاَرْضِ فَاَغْرَقْنٰهُ وَمَنْ مَّعَهٗ
جَمِيْعًا ﴿١٠٣﴾

104. Na tukawaambia baada yake wana wa Israili, "Kaeni katika nchi; na itakapokuja ahadi ya akhera, tutakuleteni (kwetu tukuhisabuni) nyote pamoja.

وَّقُلْنَا مِنْۢ بَعْدِهٖ لِبَنِيْٓ اِسْرَآءِيْلَ اسْكُنُوا الْاَرْضَ
فَاِذَا جَآءَ وَعْدُ الْاٰخِرَةِ جِئْنَا بِكُمْ لَفِيْفًا ﴿١٠٤﴾

105. Na kwa (ajili ya kuleta) haki (ulimwenguni ndio) tumeteremsha (Qurani), na kwa haki imeteremka. Na hatukukuleta ila uwe mtoaji wa khabari njema na muonyaji.

وَبِالْحَقِّ اَنْزَلْنٰهُ وَبِالْحَقِّ نَزَلَ ؕ وَمَآ اَرْسَلْنٰكَ اِلَّا مُبَشِّرًا
وَّنَذِيْرًا ﴿١٠٥﴾

106. Na Qurani tumeigawanya sehemu mbali mbali (kwa kuiteremsha kidogo kidogo) ili uwasomee watu kwa kituo; na tumeiteremsha kidogo kidogo (iwe wepesi kuhifadhika).

وَقُرْاٰنًا فَرَقْنٰهُ لِتَقْرَاَهٗ عَلَى النَّاسِ عَلٰى
مُكْثٍ وَّنَزَّلْنٰهُ تَنْزِيْلًا ﴿١٠٦﴾

107. Sema: "Iaminini (hiyo Qurani) au msiiamini. Hakika wale waliopewa ilimu (zamani) kabla hii (Qurani kuteremka), wanaposomewa (hii Qurani), huanguka kifudifudi wanasujudu

قُلْ اٰمِنُوْا بِهٖٓ اَوْ لَا تُؤْمِنُوْا ؕ اِنَّ الَّذِيْنَ اُوْتُوا الْعِلْمَ
مِنْ قَبْلِهٖٓ اِذَا يُتْلٰى عَلَيْهِمْ يَخِرُّوْنَ لِلْاَذْقَانِ
سُجَّدًا ﴿١٠٧﴾

108. Na wanasema: "Mola wetu ni mtakatifu. Hakika ahadi (inayotolewa na Mwenyezi Mungu) ya Mola wetu imetimizwa tu." (Alitoa ahadi kuwa ataleta Kitabu baada ya vitabu vya zamani, na amekileta).

وَّيَقُوْلُوْنَ سُبْحٰنَ رَبِّنَآ اِنْ كَانَ وَعْدُ رَبِّنَا
لَمَفْعُوْلًا ﴿١٠٨﴾

109. Na huanguka kifudifudi na huku wanalia (wakikumbuka makosa yao); na (Qurani) inazidi kuwaongezea unyenyekevu.

وَيَخِرُّوْنَ لِلْاَذْقَانِ يَبْكُوْنَ وَيَزِيْدُهُمْ خُشُوْعًا ﴿١٠٩﴾ السجدة

---

100. Natupigane na ubakhili wa nafsi zetu kwa kutoa katika njia zote tulizofundishwa.

107. Muradi ni kuwa Hao Manasara na Mayahudi wanaojua mambo ya dini wameiamini hii Qurani kwa kuona inawafiki yaliyosemwa na vitabu vya Mwenyezi Mungu vilivyotangulia.

110. Sema: "Muombeni (Mwenyezi Mungu) kwa (jina la) Allah au muombeni (kwa jina la) Rahman; kwa jina lolote mnalomwita (katika haya itafaa); kwani ana majina mazuri mazuri." Wala usiiseme Sala yako kwa sauti kubwa, wala usiiseme kwa sauti ndogo, bali shika njia baina ya hizo (katikati, si kwa kelele wala si kwa kimya.).

قُلِ ادْعُوا اللَّهَ أَوِ ادْعُوا الرَّحْمَٰنَ ۖ أَيًّا مَّا تَدْعُوا فَلَهُ
الْأَسْمَاءُ الْحُسْنَىٰ ۚ وَلَا تَجْهَرْ بِصَلَاتِكَ وَلَا تُخَافِتْ
بِهَا وَابْتَغِ بَيْنَ ذَٰلِكَ سَبِيلًا ﴿١١٠﴾

111. Na sema: "Sifa zote njema zinamstahikia Mwenyezi Mungu ambaye hakujifanyia mtoto wala hana mshirika (wake) katika ufalme wala hana rafiki (wa kumsaidia) kwasababu ya udhaifu wa kuhitaji. Na mtukuze kwa matukuzo makubwa (kabisa).

وَقُلِ الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي لَمْ يَتَّخِذْ وَلَدًا وَلَمْ
يَكُن لَّهُ شَرِيكٌ فِي الْمُلْكِ وَلَمْ يَكُن لَّهُ وَلِيٌّ مِّنَ
ع الذُّلِّ ۖ وَكَبِّرْهُ تَكْبِيرًا ﴿١١١﴾

---

110. Mara nyingi amesema Mwenyezi Mungu kuwa (a) Wa kuombwa ni yeye tu (b) Aombwe kwa majina yake. Ama kuombwa yeye kwa majina ya watu wengine kama Ahl Badr. Hii ni KARAHA. Ama kuombwa maiti kama dua inayoitwa Wasyla. Hayo ni HARAMU.

Tumeyabainisha haya kwa urefu katika Aya ya 180 ya *Suratul Aaraf.*

اياتها ١١٠ (١٨) سُورَةُ الْكَهْفِ مَكِّيَّةٌ (٦٩) رُكُوعَاتُهَا ١٢

*Ina Aya 110*

# SURATUL-KAHF

*Ina Makuru 12*

*(Imeteremka Makka)*

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

1. Sifa zote njema zinamstahikia Mwenyezi Mungu ambaye amemteremshia mja Wake (Nabii Muhammad) Kitabu (kitukufu hiki); wala hakukifanyia kuwa na upogo (tenge).

الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي أَنْزَلَ عَلَىٰ عَبْدِهِ الْكِتَابَ وَلَمْ يَجْعَلْ لَهُ عِوَجًا ۜ ﴿١﴾

2. Kimetengenea vizuri; ili kiwaonye watu adhabu kali itokayo Kwake (Mwenyezi Mungu) na kiwape khabari njema wale wanaoamini ambao wanafanya vitendo vizuri, ya kwamba watapata malipo mema.

قَيِّمًا لِيُنْذِرَ بَأْسًا شَدِيدًا مِنْ لَدُنْهُ وَيُبَشِّرَ الْمُؤْمِنِينَ الَّذِينَ يَعْمَلُونَ الصَّالِحَاتِ أَنَّ لَهُمْ أَجْرًا حَسَنًا ﴿٢﴾

3. Wakae humo (katika malipo hayo) milele

مَاكِثِينَ فِيهِ أَبَدًا ﴿٣﴾

4. Na kiwaonye wale wanaosema: "Mwenyezi Mungu amejifanyia mtoto."

وَيُنْذِرَ الَّذِينَ قَالُوا اتَّخَذَ اللَّهُ وَلَدًا ﴿٤﴾

5. Wao hawana ilimu juu ya (jambo) hili wala baba zao (hawana ujuzi juu ya jambo hili ila wanajisemea tu). Ni neno kubwa hilo litokalo katika vinywa vyao. Hawasemi ila uwongo tu.

مَا لَهُمْ بِهِ مِنْ عِلْمٍ وَلَا لِآبَائِهِمْ ۚ كَبُرَتْ كَلِمَةً تَخْرُجُ مِنْ أَفْوَاهِهِمْ ۚ إِنْ يَقُولُونَ إِلَّا كَذِبًا ﴿٥﴾

6. Labda utajiangamiza nafsi yako kwa kusikitikia hali yao kuwa hawaziamini hadithi hizi (unazowapa; usijihuzunishe hivyo, kama hawataki kuamini basi).

فَلَعَلَّكَ بَاخِعٌ نَفْسَكَ عَلَىٰ آثَارِهِمْ إِنْ لَمْ يُؤْمِنُوا بِهَٰذَا الْحَدِيثِ أَسَفًا ﴿٦﴾

---

Mwanzo wa Sura hii wametia tena ukafiri wao wa kumkanusha Mwenyezi Mungu kwa anayoyasema. Wanasema hapa kuwa kisa cha Nabii Musa alichokisimulia Mwenyezi Mungu cha kwenda Nabii Musa kuonana na Nabii Al Khidhr — na akaonana naye na yakatokea yaliyotokea — ni ndoto (njozi), kama walivyosema kuwa Israi ya Mtume Muhammad na Miiraji yake ni ndoto pia! Na vile vile kisa cha kulala Ahlil Kahf muda wa miaka 300 na kitu, kisha wakafufuliwa. Wanasema kuwa muradi wake Waislamu watatawala; kisha na Wakristo nao, watatawala. Wakasema haya katika Aya walizozifanya za 19 mpaka 23. Wao hamu yao ni kumpinga Mwenyezi Mungu tu na dini yake ya haki. Mungu hatasimama nao. Na hayo waliyoyajaza humo mwanzo wa Sura hii na katika maelezo yake yote, ni farumu tu za uwongo na upotezaji. Na zote wanasema zimekhusu utawala wa Kiislamu na utawala wa Wakristo. Nao ni uwongo mtupu. Wanapoteza makusudi.

1. Tumebainisha mara nyingi kuwa Qurani haina kwenda upogo (kwenda upande) hata chembe kabisa. Hapana lolote lililosemea na Qurani likaonekana—kwa hoja na dalili—kuwa hili si barabara. Tangu ilipoanza kuteremka mpaka leo. Kama analo mtu naatuletee au ampelekee yoyote amtakaye katika wanavyuoni.

5. Hao wanaosema waungu watatu au wawili au zaidi hawana hoja yoja yoyote, la ya kiakili wala ya kidini. Wanajisemea mafamba tu, wanawafuata makafiri wa nyuma waliotangulia huko; kama alivyobainisha haya Mwenyezi Mungu katika Aya ya 30 ya *SuratutuTawba.*

6. Mtume alikuwa na hamu kubwa kabisa isiyokuwa na mfano katika kutaka watu waongoke hata akijitia katika mashaka makubwa ya kumpelekea kuhiliki, kama tulivyobainisha katika Aya ya 128 ya *Suratut Tawba.*

7. Kwa hakika tumevifanya vilivyoko juu ya ardhi viwe pambo lake, ili tuwatazame ni nani katika wao (viumbe) wenye vitendo vizuri zaidi.

إِنَّا جَعَلْنَا مَا عَلَى الْأَرْضِ زِينَةً لَّهَا لِنَبْلُوَهُمْ أَيُّهُمْ أَحْسَنُ عَمَلًا ﴿٧﴾

8. Na hakika sisi ndio tunaofanya hivyo vilivyoko juu yake kuwa (baada yake) ardhi kame (kavu isiyokuwa na chochote).

وَإِنَّا لَجَاعِلُونَ مَا عَلَيْهَا صَعِيدًا جُرُزًا ﴿٨﴾

9. Je! Unafikiri ya kwamba (wale) watu wa Pangoni na (wenye habari) zile zilizoandikwa (vitabuni) walikuwa ajabu katika ajabu zetu?

أَمْ حَسِبْتَ أَنَّ أَصْحَابَ الْكَهْفِ وَالرَّقِيمِ كَانُوا مِنْ آيَاتِنَا عَجَبًا ﴿٩﴾

10. Vijana hao walipokimbilia katika pango na wakasema: "Mola wetu; tupe rehema zinazotoka kwako na tutengenezee uwongofu katika (kila) jambo letu."

إِذْ أَوَى الْفِتْيَةُ إِلَى الْكَهْفِ فَقَالُوا رَبَّنَا آتِنَا مِن لَّدُنكَ رَحْمَةً وَهَيِّئْ لَنَا مِنْ أَمْرِنَا رَشَدًا ﴿١٠﴾

11. Tukaziba masikio yao (wakalala hawasikii habari yoyote) katika pango hiyo kwa idadi ya myaka mingi

فَضَرَبْنَا عَلَىٰ آذَانِهِمْ فِي الْكَهْفِ سِنِينَ عَدَدًا ﴿١١﴾

12. Kisha tukawafufua ili tujulishe ni lipi katika makundi mawili lililohisabu sawasawa muda waliokaa (hawa vijana wa pangoni).

ثُمَّ بَعَثْنَاهُمْ لِنَعْلَمَ أَيُّ الْحِزْبَيْنِ أَحْصَىٰ لِمَا لَبِثُوا أَمَدًا ﴿١٢﴾

13. Sisi tunakusimulia habari zao kwa kweli. Hakika wao walikuwa ni vijana waliomuamini Mola wao. Nasi tukawazidisha uwongofu.

نَّحْنُ نَقُصُّ عَلَيْكَ نَبَأَهُم بِالْحَقِّ ۚ إِنَّهُمْ فِتْيَةٌ آمَنُوا بِرَبِّهِمْ وَزِدْنَاهُمْ هُدًى ﴿١٣﴾

14. Na tukazitia nguvu nyoyo zao walipoSimama (mbele ya mfalme wao kafiri na mbele ya watu wote) wakasema: "Mola wetu ni Mola wa mbingu na ardhi. Hatutamuabudu kabisa mungu mwingine badala yake. (Hapo) bila shaka tutakuwa tumesema uovu uliyopindukia kiasi."

وَرَبَطْنَا عَلَىٰ قُلُوبِهِمْ إِذْ قَامُوا فَقَالُوا رَبُّنَا رَبُّ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ لَن نَّدْعُوَ مِن دُونِهِ إِلَٰهًا ۖ لَّقَدْ قُلْنَا إِذًا شَطَطًا ﴿١٤﴾

15. "Hawa watu wetu wamefanya waungu (wengine) badala yake. Kwa nini hawaleti juu yao dalili iliyo dhahiri (ya kuonyesha kuwa wao ni waungu)? Basi ni nani dhalimu mkubwa kuliko yule amzuliaye Mwenyezi Mungu uwongo?"

هَٰؤُلَاءِ قَوْمُنَا اتَّخَذُوا مِن دُونِهِ آلِهَةً ۖ لَّوْلَا يَأْتُونَ عَلَيْهِم بِسُلْطَانٍ بَيِّنٍ ۖ فَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنِ افْتَرَىٰ عَلَى اللَّهِ كَذِبًا ﴿١٥﴾

16. (Na wakaambiana hivi) "Na mlipokuwa mumejitenga nao na vile wanavyoviabudu badala ya Mwenyezi Mungu, basi kimbilieni pangoni; atakufungulieni Mola wenu (huko) rehema zake na kukufanyieni wepesi katika mambo yenu (yote)."

وَإِذِ اعْتَزَلْتُمُوهُمْ وَمَا يَعْبُدُونَ إِلَّا اللَّهَ فَأْوُوا إِلَى الْكَهْفِ يَنشُرْ لَكُمْ رَبُّكُم مِّن رَّحْمَتِهِ وَيُهَيِّئْ لَكُم مِّنْ أَمْرِكُم مِّرْفَقًا ﴿١٦﴾

---

9. Hapa inatajwa habari ya hao vijana wanaojulikana kwa jina la *As'habul Kahf* (Vijana wa Pangoni). Hao ni vijana walioamini dini ya haki katika nchi fulani na hali ya kuwa Mfalme na watu wote wa nchi hiyo hawaiamini dini hiyo ya haki. Wakataka kuwadhuru. Basi wakenda wakajificha Pangoni pamoja na mbwa wao. Humo ukawachukua usingizi muda wa myaka 300 na zaidi.

Baada ya hiyo myaka 300 ndipo walipozindukana; wenyewe wanadhani wamelala siku moja hivi au chini kuliko siku moja; kumbe wamelala myaka 300. Mambo ya nchi ile yote yaligeuka na ikawa wote wanaifuata ile dini waliotangulia kufuata wao. Tumebainisha katika Aya ya 83 ya *Surat Yunus* kuwa vijana ndio wanaokuwa wepesi kufuata haki inapokuja.

17. (Na ikawa hivi:–) Unaliona jua linapochomoza (linapopanda) linapita mbali na pango yao kwa upande wa kulia. Na linapokuwa linakuchwa linawakata upande wa kushoto (bila kuwakabili sawa sawa). Nao wamo katika uwazi ndani yake humo. Hizo ni katika ishara za (uweza wa) Mwenyezi Mungu. Ambaye Mwenyezi Mungu anamuongoza basi yeye ndiye aliyeongoka; na anayemwachia kupotea, basi hutampatia mlinzi mwongozi.

وَتَرَى الشَّمْسَ اِذَا طَلَعَتْ تَّزٰوَرُ عَنْ كَهْفِهِمْ
ذَاتَ الْيَمِيْنِ وَاِذَا غَرَبَتْ تَّقْرِضُهُمْ
ذَاتَ الشِّمَالِ وَهُمْ فِيْ فَجْوَةٍ مِّنْهُ ۚ ذٰلِكَ مِنْ
اٰيٰتِ اللّٰهِ ۗ مَنْ يَّهْدِ اللّٰهُ فَهُوَ الْمُهْتَدِ ۚ وَمَنْ يُّضْلِلْ
فَلَنْ تَجِدَ لَهٗ وَلِيًّا مُّرْشِدًا ﴿١٧﴾

18. Na unawadhani wamacho na hali wamelala. Na tunawageuza upande wa kulia na upande wa kushoto, (wanapogaragara usingizini). Na mbwa wao kanyosha mikono yake kizingitini. Kama ungewaona hakika ungegeuka upesi kuwakimbia, na hakika ungejazwa khofu juu yao.

وَتَحْسَبُهُمْ اَيْقَاظًا وَّهُمْ رُقُوْدٌ ۖ وَّنُقَلِّبُهُمْ ذَاتَ
الْيَمِيْنِ وَذَاتَ الشِّمَالِ ۖ وَكَلْبُهُمْ بَاسِطٌ ذِرَاعَيْهِ
بِالْوَصِيْدِ ۚ لَوِ اطَّلَعْتَ عَلَيْهِمْ لَوَلَّيْتَ مِنْهُمْ فِرَارًا
وَّلَمُلِئْتَ مِنْهُمْ رُعْبًا ﴿١٨﴾

19. Basi namna hivi (katika hali hii) tuliwafufua (tuliwainua) ili waulizane baina yao. Akasema msemaji katika wao: "Mumekaa muda gani?" Wakasema: "Tumekaa siku moja au sehemu ya siku." (Wengine) wakasema: "Mola wenu anajuwa zaidi muda mliokaa. Basi mtumeni mmoja wenu pamoja na fedha yenu hii mjini na akatazame chakula chake kipi ni tahara zaidi akuleteeni katika chakula hicho. Naafanye mambo haya kwa busara wala asikutajeni kabisa kwa yoyote."

وَكَذٰلِكَ بَعَثْنٰهُمْ لِيَتَسَآءَلُوْا بَيْنَهُمْ ۚ قَالَ قَآئِلٌ
مِّنْهُمْ كَمْ لَبِثْتُمْ ۚ قَالُوْا لَبِثْنَا يَوْمًا اَوْ بَعْضَ يَوْمٍ ۚ
قَالُوْا رَبُّكُمْ اَعْلَمُ بِمَا لَبِثْتُمْ ۚ فَابْعَثُوْا اَحَدَكُمْ
بِوَرِقِكُمْ هٰذِهٖۤ اِلَى الْمَدِيْنَةِ فَلْيَنْظُرْ اَيُّهَاۤ اَزْكٰى
طَعَامًا فَلْيَاْتِكُمْ بِرِزْقٍ مِّنْهُ وَلْيَتَلَطَّفْ وَلَا
يُشْعِرَنَّ بِكُمْ اَحَدًا ﴿١٩﴾

20. "Kwani wao wakikujueni mlipo watakupigeni mawe au watakurudisheni katika dini yao; na hapo hamtafaulu abadan." (Wao wakidhani watu wa nchi hiyo bado makafiri).

اِنَّهُمْ اِنْ يَّظْهَرُوْا عَلَيْكُمْ يَرْجُمُوْكُمْ اَوْ يُعِيْدُوْكُمْ
فِيْ مِلَّتِهِمْ وَلَنْ تُفْلِحُوْۤا اِذًا اَبَدًا ﴿٢٠﴾

21. (Lakini walitambulikana ilipoonekana sarfa ya zamani kabisa) na namna hivi tuliwatambulisha (kwa watu) ili wapate kujua ya kwamba ahadi ya Mwenyezi Mungu (ya kufufuliwa viumbe) ni kweli, na ya kwamba Kiama hakina shaka. (Na kumbukeni) walipozozana baina yao juu ya jambo lao (hawa waliokutanika hapa pangoni) wakasema wengine "Jengeni jengo juu yao (wasipate kupita watu kuja kuwachungulia). Mola wao anawajua vyema. (Basi inatosha)". Wakasema wale waloshinda katika shauri lao; "Bila shaka sisi tutajenga msikiti juu yao." (Yaani katika pango yao).

وَكَذٰلِكَ اَعْثَرْنَا عَلَيْهِمْ لِيَعْلَمُوْۤا اَنَّ وَعْدَ
اللّٰهِ حَقٌّ وَّاَنَّ السَّاعَةَ لَا رَيْبَ فِيْهَا ۚ اِذْ يَتَنَازَعُوْنَ
بَيْنَهُمْ اَمْرَهُمْ فَقَالُوا ابْنُوْا عَلَيْهِمْ بُنْيَانًا ۚ رَبُّهُمْ
اَعْلَمُ بِهِمْ ۚ قَالَ الَّذِيْنَ غَلَبُوْا عَلٰۤى اَمْرِهِمْ لَنَتَّخِذَنَّ
عَلَيْهِمْ مَّسْجِدًا ﴿٢١﴾

---

18,22. Kwa ajili ya kukimbia kwao muujiza wa Mwenyezi Mungu wa kufufua waliokufa na kuwafisha tena, wamegeuza kabisa maelezo ya Aya hizi. Wametia yale yale mapotezo yao. Wakasema kuwa muradi wa hayo ni kuwa Waislamu wataregea, na Wakristo watatawala dunia. Haya! Wenyewe siku ya Kiama watajionea.

21. Iliweza kutambulikana kuwa ahadi ya Mwenyezi Mungu ya kufufua viumbe ni kweli kwa kuonekana kufufuka hao watu waliolala zaidi kuliko miaka 300.

22. (Wengine) wanasema: "Walikuwa watu watatu wa nne wao ni mbwa wao." Na (wengine) wanasema, "Walikuwa watano, wa sita wao ni mbwa wao." (Wanasema) kwa kuvurumiza (tu) kwa wasioyajuwa. Na (wengine) wanasema, "Walikuwa saba, na wa nane wao ni mbwa wao." Sema: "Mola wangu ndiye ajuaye sawasawa hisabu yao." Hakuna anayewajua (hakika yao) isipokuwa wachache tu. Basi usibishane (usishindane) juu yao ila kwa mabishano ya juu juu tu hivi (kwani hapana faida juu ya mabishano ya kuwa walikuwa wangapi). Wala usiulize khabari zao kwa yoyote yule. (Mwenyezi Mungu ameshakutajia. Basi hivi alivyokutajia ndio ndivyo).

سَيَقُولُونَ ثَلَاثَةٌ رَّابِعُهُمْ كَلْبُهُمْ وَيَقُولُونَ
خَمْسَةٌ سَادِسُهُمْ كَلْبُهُمْ رَجْمًا بِالْغَيْبِ
وَيَقُولُونَ سَبْعَةٌ وَثَامِنُهُمْ كَلْبُهُمْ قُل رَّبِّي أَعْلَمُ
بِعِدَّتِهِم مَّا يَعْلَمُهُمْ إِلَّا قَلِيلٌ فَلَا تُمَارِ فِيهِمْ
إِلَّا مِرَاءً ظَاهِرًا وَلَا تَسْتَفْتِ فِيهِم مِّنْهُمْ أَحَدًا ﴿٢٢﴾

23. Wala usiseme kamwe kwa lolote lile kuwa: "Nitalifanya kesho."

وَلَا تَقُولَنَّ لِشَيْءٍ إِنِّي فَاعِلٌ ذَٰلِكَ غَدًا ﴿٢٣﴾

24. Isipokuwa (uongeze) "Inshallah (Mwenyezi Mungu akipenda)." Na umkumbuke Mola wako unaposahau na sema "Asaa Mola wangu ataniongoza njia iliyo karibu zaidi na uwongofu kuliko hii (niliyopita)."

إِلَّا أَن يَشَاءَ اللَّهُ وَاذْكُر رَّبَّكَ إِذَا نَسِيتَ
وَقُلْ عَسَىٰ أَن يَهْدِيَنِ رَبِّي لِأَقْرَبَ مِنْ هَٰذَا
رَشَدًا ﴿٢٤﴾

25. Na walikaa katika pango yao myaka mia tatu, na wakazidisha (myaka) tisa.

وَلَبِثُوا فِي كَهْفِهِمْ ثَلَاثَ مِائَةٍ سِنِينَ وَازْدَادُوا تِسْعًا ﴿٢٥﴾

---

Baada ya kwisha kujuwana na watu na kujulikana wao, walikufa tena. Sasa walikufa khasa sio kulala tu. Basi ikapitishwa shauri la kujengewa msikiti katika Pango yao hiyo.

Imesemwa "Walioshinda katika shauri lao', ndio waliosema wajengewe msikiti. Haya ni kuonyesha kuwa haifai (a) Makaburi kuyajengea misikiti — kuzikwa mtu kisha ukajengwa msikiti, ikawa hilo kaburi liko ndani ya msikiti. Au ndani ya msikiti likachimbwa kaburi akazikwa maiti: Yote mawili haya haramu kubwa kabisa.

Wenye kufanya hivi Mwenyezi Mungu amewalaani kama ilivyobainishwa katika Hadithi za Mtume zinazokubaliwa.

Na watu wanayafanya haya juu ya kuambiwa kuwa wenye kufanya hayo Mwenyezi Mungu anawalaani, kama ilivyo katika Hadithi. Lakini hawasikii.

Na vile vile wanakatazwa kumzika maiti hata nje ya misikiti, khasa yakiwa kibla makaburi hayo. Na kila siku watu wanayafanya, khasa akifa mtu mkubwa wastani. Ama mkubwa kabisa wanamtia ndani ya msikiti. Nawafanye tu, na laana zitawashukia maisha yao hata baada ya kufa kwao.

Na akisema mtu kaburi la Mtume limo ndani ya Msikiti, ataambiwa "Limefanywa liwe ndani ya Msikiti zama za wafalme wajeuri wa Bani Umayya zama za Al Walyd bin Abdil Malik bin Marwan". Wakapinga baadhi ya watoto wa Masahaba sana sana. Nawakaadhibiwa kwa kupinga huko, hata wengine wakafa katika hizo adhabu, kama Bwana Khabbab bin Abdulla bin Zubeyr.

Na vile vile wanalaaniwa wanaoyawashia taa hayo makaburi, kwa shahada ya Hadithi za Mtume zinazokubaliwa. Na kila wakiambiwa hawasikii. Khiari yao. Bali vile vile haramu (a) kuyajengea japokuwa kuyazungushia vikuta vidogo; seuze kuyajengea Makuba.

Wala asiseme mtu kuwa "Mbona kaburi la Mtume limejengewa *Qubbatul Khadhraa?*" Akisema hivyo ataonyesha ujinga wake kuwa hajui kuwa kuba hilo limejengwa katika karne ya Saba na mfalme mjeuri katika kizazi cha Salahud Din Al Ayyuby. Na wanavyuoni wa haki wakapiga kelele sana kukataza; lakini wajeuri hao hawakuwasikiliza.

23. Kwani huwezi kujua kuwa utaweza kulifanya au hutaweza. Unaweza wapi kujua yatakayotokeya kesho?

25. Wengine wanasema kuwa maana ya Aya hii ni kuwa kwa hisabu ya myaka ya jua wamelala miaka mia tatu na kwa hisabu ya mwendo wa mwezi myaka mia tatu na tisa.

26. Sema: "Mwenyezi Mungu anajuwa barabara muda waliokaa."[26] Ni zake (peke yake Mwenyezi Mungu) siri za mbingu na ardhi. Kuona kulioje kwa Mwenyezi Mungu na kusikia kwake; Nao hawana mlinzi badala yake (Mwenyezi Mungu) wala yeye hamshirikishi yoyote katika hukumu Zake.

قُلِ اللّٰهُ اَعْلَمُ بِمَا لَبِثُوْا ۚ لَهٗ غَيْبُ السَّمٰوٰتِ
وَالْاَرْضِ ؕ اَبْصِرْ بِهٖ وَاَسْمِعْ ؕ مَا لَهُمْ مِّنْ دُوْنِهٖ
مِنْ وَّلِيٍّ ۫ وَّلَا يُشْرِكُ فِيْ حُكْمِهٖۤ اَحَدًا ﴿٢٦﴾

27. Na usome uliyoletewa Wahyi (yaliyofunuliwa kwako) katika kitabu cha Mola wako. Hakuna awezaye kubadilisha maneno yake. Nawe hutapata makimbilio ya kumkimbia yeye (Mwenyezi Mungu) asikupate.

وَاتْلُ مَاۤ اُوْحِيَ اِلَيْكَ مِنْ كِتَابِ رَبِّكَ ۚ
لَا مُبَدِّلَ لِكَلِمٰتِهٖ ۚ وَلَنْ تَجِدَ مِنْ دُوْنِهٖ
مُلْتَحَدًا ﴿٢٧﴾

28. Na ujiweke pamoja na wale wanaomuabudu Mola wao asubuhi na jioni, hali ya kuwa wanataka radhi yake. Wala macho yako yasiwaruke (hawa ukawatafuta wengine), kwa kutaka pambo la maisha ya dunia. Wala usiwatii wale ambao tumezighafilisha nyoyo zao wakafuata matamanio yao, na mambo yao yakawa yamepita mipaka (yaani makafiri).

وَاصْبِرْ نَفْسَكَ مَعَ الَّذِيْنَ يَدْعُوْنَ رَبَّهُمْ
بِالْغَدٰوةِ وَالْعَشِيِّ يُرِيْدُوْنَ وَجْهَهٗ وَلَا
تَعْدُ عَيْنٰكَ عَنْهُمْ ۚ تُرِيْدُ زِيْنَةَ الْحَيٰوةِ الدُّنْيَا ۚ
وَلَا تُطِعْ مَنْ اَغْفَلْنَا قَلْبَهٗ عَنْ ذِكْرِنَا وَاتَّبَعَ
هَوٰىهُ وَكَانَ اَمْرُهٗ فُرُطًا ﴿٢٨﴾

29. Na sema: "Huu ni ukweli uliotoka kwa Mola wenu, basi anayetaka naamini na anayetaka naakufuru." Hakika tumewaandalia (tumewawekea tayari) madhalimu moto ambao kuta zake zitawazunguka. Na wakiomba msaada (kwa kiu kubwa iliyowashika), watasaidiwa kwa (kupewa) maji kama ya shaba iliyoyayushwa itayoziunguza nyuso (zao). Kinywaji kibaya kilioje hicho. Na mahala pabaya palioje.

وَقُلِ الْحَقُّ مِنْ رَّبِّكُمْ ۚ فَمَنْ شَآءَ فَلْيُؤْمِنْ وَّمَنْ
شَآءَ فَلْيَكْفُرْ ۚ اِنَّاۤ اَعْتَدْنَا لِلظّٰلِمِيْنَ نَارًا ۙ اَحَاطَ
بِهِمْ سُرَادِقُهَا ؕ وَاِنْ يَّسْتَغِيْثُوْا يُغَاثُوْا بِمَآءٍ
كَالْمُهْلِ يَشْوِي الْوُجُوْهَ ؕ بِئْسَ الشَّرَابُ ؕ وَسَآءَتْ
مُرْتَفَقًا ﴿٢٩﴾

30. Hakika wale walioamini na kufanya vitendo vizuri (tutawalipa kwa mema yao hayo). Hakika sisi hatupotezi ujira wa wale wanaofanya vitendo vizuri.

اِنَّ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ اِنَّا لَا نُضِيْعُ
اَجْرَ مَنْ اَحْسَنَ عَمَلًا ﴿٣٠﴾

31. Hao watapata mabustani ya milele, yanayopita mito (ya maji) mbele yake. Humo watapambwa kwa mavazi ya mikononi ya dhahabu na watavaa nguo za kijani za hariri laini na za hariri nzito; wanaengemea humo juu ya vitanda vilivyopambwa (makochi). Ni malipo mazuri yaliyoje hayo! Na mahali bora palioje hapo (pa kupumzikia).

اُولٰٓئِكَ لَهُمْ جَنّٰتُ عَدْنٍ تَجْرِيْ مِنْ تَحْتِهِمُ الْاَنْهٰرُ
يُحَلَّوْنَ فِيْهَا مِنْ اَسَاوِرَ مِنْ ذَهَبٍ وَّيَلْبَسُوْنَ ثِيَابًا
خُضْرًا مِّنْ سُنْدُسٍ وَّاِسْتَبْرَقٍ مُّتَّكِـِٕيْنَ فِيْهَا عَلَى الْاَ
رَآئِكِ ؕ نِعْمَ الثَّوَابُ ؕ وَحَسُنَتْ مُرْتَفَقًا ﴿٣١﴾

---

26. Katika Aya waliyoifanya ya 28 wametia ukafiri wao tena wa kusema kuwa Nabii Isa amesulubiwa. Na tumejibu ukafiri huu katika Aya ya 54 ya *Surat Aali Imran*.

27,29. Wamekoroga kusudi makusudio ya Aya hizi walizozifanya ni za 28 na 29. Wanaona — kama kila mtu anavyoona — kuwa kwa Aya hizi Mtume anaamrishwa awasemeze wabaya walio katika zama zake; wao wanasema watu hawa watakuwa katika zama za Imamu Mahdi. Na yote haya ni kwa ajili ya kutaka kumpachikiza huyo mtu wao. Wanampachikiza kila mahala patukufu — ingawa hapachikiziki. Mara wanamdaia (a) Unabii Isa (Al Masihul Mauud); mara (b) Utume tu. Sasa (c) Uimam Mahd (Huyu Muhudi). Na yote hayo ni uwongo na ni ukafiri: (i) Kujigamba nao mtu na (ii) kumgambia. Wanapindua dhahiri ya Qurani hivi kimachomacho bila ya kujali wala kubali.

28. Wakubwa wa Kikureshi waliokuwa makafiri walimwambia Mtume 'Ukitaka tukufuate basi wafukuze hao maskini waliokufuata.

32. Na wapigie mfano wa watu wawili: mmoja wao tulimfanyia (tulimpa) mabustani mawili ya mizabibu, na tukaizungushia mitende, na pia katikati yake tukatia miti ya nafaka (nyingine).

وَاضْرِبْ لَهُم مَّثَلًا رَّجُلَيْنِ جَعَلْنَا لِأَحَدِهِمَا جَنَّتَيْنِ مِنْ أَعْنَابٍ وَحَفَفْنَاهُمَا بِنَخْلٍ وَجَعَلْنَا بَيْنَهُمَا زَرْعًا ﴿٣٢﴾

33. Haya mabustani mawili yote yalijaa matunda yake wala hayakupunguza chochote (katika uzazi wake); na ndani yake tukapitisha mito

كِلْتَا الْجَنَّتَيْنِ آتَتْ أُكُلَهَا وَلَمْ تَظْلِم مِّنْهُ شَيْئًا ۚ وَفَجَّرْنَا خِلَالَهُمَا نَهَرًا ﴿٣٣﴾

34. Na akawa na mali mengine (pia). Basi akamwambia mwenzake na hali ya kuwa akibishana naye, "Mimi nina mali nyingi kuliko wewe na (nina) nguvu zaidi kwa ajili ya wafuasi (nilio nao)."

وَكَانَ لَهُ ثَمَرٌ ۚ فَقَالَ لِصَاحِبِهِ وَهُوَ يُحَاوِرُهُ أَنَا أَكْثَرُ مِنكَ مَالًا وَأَعَزُّ نَفَرًا ﴿٣٤﴾

35. Na akaingia katika bustani yake na hali ya kuwa anajidhulumu nafsi yake (kwa maasia) akasema: "Sidhani abadan kuwa (bustani) hili litaharibika"

وَدَخَلَ جَنَّتَهُ وَهُوَ ظَالِمٌ لِّنَفْسِهِ ۚ قَالَ مَا أَظُنُّ أَن تَبِيدَ هَٰذِهِ أَبَدًا ﴿٣٥﴾

36. "Wala sidhani kuwa Kiama kitatokea. Na kama (kitatokea hicho Kiama) nikarudishwa kwa Mola wangu, bila shaka nitakuta kikao chema kuliko hiki (alichonipa ulimwenguni. Siku njema huonekana asubuhi. Kama nilivyopata huku, na huko nitapata)

وَمَا أَظُنُّ السَّاعَةَ قَائِمَةً ۚ وَلَئِن رُّدِدتُّ إِلَىٰ رَبِّي لَأَجِدَنَّ خَيْرًا مِّنْهَا مُنقَلَبًا ﴿٣٦﴾

37. Mwenzake akamwambia na hali ya kuwa anamjibu: "Je! Unamkufuru (na unakanusha neema za) yule aliyekuumba kwa udongo, tena kwa tone la manii, kisha akakufanya mtu kamili?"

قَالَ لَهُ صَاحِبُهُ وَهُوَ يُحَاوِرُهُ أَكَفَرْتَ بِالَّذِي خَلَقَكَ مِن تُرَابٍ ثُمَّ مِن نُّطْفَةٍ ثُمَّ سَوَّاكَ رَجُلًا ﴿٣٧﴾

38. "Lakini (mimi namuamini) yeye Mwenyezi Mungu (tu kuwa) ndiye Mola wangu, wala simshirikishi Mola wangu na yoyote."

لَّٰكِنَّا هُوَ اللَّهُ رَبِّي وَلَا أُشْرِكُ بِرَبِّي أَحَدًا ﴿٣٨﴾

39. "Na lau ulipoingia katika bustani yako (hii) ulisema "Hivi nilivyonavyo amenitakia Mwenyezi Mungu. Nguvu hazipatikani ila kwa (kupewa na) Mwenyezi Mungu. (Ungesema hivi ingekuwa bora). Kama unaniona mimi nina mali kidogo na watoto wachache kuliko wewe."

وَلَوْلَا إِذْ دَخَلْتَ جَنَّتَكَ قُلْتَ مَا شَاءَ اللَّهُ لَا قُوَّةَ إِلَّا بِاللَّهِ ۚ إِن تَرَنِ أَنَا أَقَلَّ مِنكَ مَالًا وَوَلَدًا ﴿٣٩﴾

40. "Basi hwenda Mola wangu akanipa kilicho bora kuliko bustani yako na kuipelekea (hiyo bustani yako) mapigo ya radi kutoka mbinguni na ikawa ardhi tupu inayotelezesha (isiyokuwa na mmea)"

فَعَسَىٰ رَبِّي أَن يُؤْتِيَنِ خَيْرًا مِّن جَنَّتِكَ وَيُرْسِلَ عَلَيْهَا حُسْبَانًا مِّنَ السَّمَاءِ فَتُصْبِحَ صَعِيدًا زَلَقًا ﴿٤٠﴾

41. "Au maji yake yakawa yenye kuzama hata usiweze kuyapata."

أَوْ يُصْبِحَ مَاؤُهَا غَوْرًا فَلَن تَسْتَطِيعَ لَهُ طَلَبًا ﴿٤١﴾

42. Basi matunda (mali) yake yakabambwa (yakaangamizwa) na akawa anapinduapindua viganja

وَأُحِيطَ بِثَمَرِهِ فَأَصْبَحَ يُقَلِّبُ كَفَّيْهِ عَلَىٰ

---

32, 44. Katika Aya hizi walizozifanya za 33-45 Mwenyezi Mungu anasimulia habari za watu wawili waliopita; wao wanasema kuwa ni habari ya mambo yatakayokuja baina ya Uislamu na Ukristo.

مَا أَنْفَقَ فِيهَا وَهِيَ خَاوِيَةٌ عَلَىٰ عُرُوشِهَا
وَيَقُولُ يَا لَيْتَنِي لَمْ أُشْرِكْ بِرَبِّي أَحَدًا ﴿٤٢﴾

vyake (anasikitika) kwa ajili ya alichokigharimia (yale mabustani). Ikawa miti yake imeanguka juu ya chanja zake, na akawa anasema: "Laiti nisingalimshirikisha Mola wangu na yoyote!"

وَلَمْ تَكُنْ لَهُ فِئَةٌ يَنْصُرُونَهُ مِنْ دُونِ اللَّهِ
وَمَا كَانَ مُنْتَصِرًا ﴿٤٣﴾

43. Wala hakuwa na watu wa kumsaidia baada ya (kumkosa) Mwenyezi Mungu, wala mwenyewe kujisaidia.

هُنَالِكَ الْوَلَايَةُ لِلَّهِ الْحَقِّ ۚ هُوَ خَيْرٌ ثَوَابًا وَخَيْرٌ
عُقْبًا ﴿٤٤﴾ ع

44. Huko (akhera) ufalme ni wa Mwenyezi Mungu tu aliyoko daima. Yeye ndiye bora kwa malipo na (ndiye) bora wa (kuleta) matokeo mazuri.

وَاضْرِبْ لَهُمْ مَثَلَ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا كَمَاءٍ أَنْزَلْنَاهُ
مِنَ السَّمَاءِ فَاخْتَلَطَ بِهِ نَبَاتُ الْأَرْضِ فَأَصْبَحَ
هَشِيمًا تَذْرُوهُ الرِّيَاحُ ۗ وَكَانَ اللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ
مُقْتَدِرًا ﴿٤٥﴾

45. Na wapigie mfano wa maisha ya dunia: (Maisha ya dunia) ni kama maji tunayoyateremsha kutoka mawinguni; kisha huchanganyika nayo (maji hayo) mimea ya ardhi (ikastawi); kisha (baadaye) ikawa (mimea hiyo) majani makavu yaliyokatikakatika ambayo upepo huyarusha huku na huko. Na Mwenyezi Mungu Ana uweza juu ya kila kitu.

الْمَالُ وَالْبَنُونَ زِينَةُ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا ۖ وَالْبَاقِيَاتُ
الصَّالِحَاتُ خَيْرٌ عِنْدَ رَبِّكَ ثَوَابًا وَخَيْرٌ أَمَلًا ﴿٤٦﴾

46. Mali na watoto ni pambo la maisha ya dunia. Na vitendo vizuri vibakiavyo ndivyo bora mbele ya Mola wako kwa malipo na tumaini bora (kuliko hayo mali na watoto).

وَيَوْمَ نُسَيِّرُ الْجِبَالَ وَتَرَى الْأَرْضَ بَارِزَةً
وَحَشَرْنَاهُمْ فَلَمْ نُغَادِرْ مِنْهُمْ أَحَدًا ﴿٤٧﴾

47. Na (wakumbushe) siku tutakayoiendesha milima (angani inaruka kama sufi), na utaiona ardhi iwazi (imenyoka moja kwa moja, haikuzibwa kwa milima wala miti wala vinginevyo). Nasi (siku hiyo) tutawafufua (viumbe wote) wala hatutamuacha hata mmoja katika wao.

وَعُرِضُوا عَلَىٰ رَبِّكَ صَفًّا لَقَدْ جِئْتُمُونَا كَمَا
خَلَقْنَاكُمْ أَوَّلَ مَرَّةٍ ۚ بَلْ زَعَمْتُمْ أَلَّنْ نَجْعَلَ لَكُمْ
مَوْعِدًا ﴿٤٨﴾

48. Na watahudhurishwa mbele ya Mola wako safu safu (na wataambiwa): "Bila shaka mumetujia kama tulivyokuumbeni mara ya kwanza. Bali (Lakini) mlidhani ya kuwa hatukukuwekeeni miadi (hii).

وَوُضِعَ الْكِتَابُ فَتَرَى الْمُجْرِمِينَ مُشْفِقِينَ
مِمَّا فِيهِ وَيَقُولُونَ يَا وَيْلَتَنَا مَالِ هَٰذَا الْكِتَابِ
لَا يُغَادِرُ صَغِيرَةً وَلَا كَبِيرَةً إِلَّا أَحْصَاهَا ۚ وَ
وَجَدُوا مَا عَمِلُوا حَاضِرًا ۗ وَلَا يَظْلِمُ رَبُّكَ
أَحَدًا ﴿٤٩﴾ ع

49. Na madaftari yatawekwa (mbele yao). Utawaona wabaya wanavyoogopa kwa sababu ya yale yaliyomo (madaftarini); na watasema: "Ole wetu! Eee kuangamia kwetu leo)! Namna gani madaftari haya! Haliachi dogo wala kubwa ila yamelidhibiti (yameliandika)!" Na watakuta yote yale waliyoyafanya yamehudhuria hapo; na Mola wako hamdhulumu yoyote.

وَإِذْ قُلْنَا لِلْمَلَائِكَةِ اسْجُدُوا لِآدَمَ فَسَجَدُوا إِلَّا
إِبْلِيسَ كَانَ مِنَ الْجِنِّ فَفَسَقَ عَنْ أَمْرِ رَبِّهِ ۗ

50. Na (kumbukeni) tulipowaambia Malaika, msujudieni Adamu. Basi wakamsujudia isipokuwa Ibilisi; yeye alikuwa miongoni mwa majini, na akavunja amri ya Mola wake. Je! mnamfanya yeye

44. Ya kumfaa mtu huko ni yale ya kumfurahisha Mwenyezi Mungu.

na kizazi chake kuwa marafiki (zenu) badala yangu, hali wao ni maadui zenu? Ni mbaya kabisa kwa madhalimu badala (hii).

أَفَتَتَّخِذُونَهُ وَذُرِّيَّتَهُ أَوْلِيَاءَ مِن دُونِي وَهُمْ
لَكُمْ عَدُوٌّ ۚ بِئْسَ لِلظَّالِمِينَ بَدَلًا ﴿٥٠﴾

51. Sikuwashuhudisha kuumbwa kwa mbingu na ardhi wala kuumbwa kwa nafsi zao; wala sikuwafanya wapotezao kuwa wasaidizi (wangu).

مَّا أَشْهَدتُّهُمْ خَلْقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَلَا خَلْقَ
أَنفُسِهِمْ وَمَا كُنتُ مُتَّخِذَ الْمُضِلِّينَ عَضُدًا ﴿٥١﴾

52. Na (kumbukeni) siku atakayosema (Mwenyezi Mungu) "Waiteni washirika wangu ambao mlidai (kuwa washirika wangu.)" Basi watawaita, lakini hawatawaitikia; na tutatia kizuwizi baina yao, (hawawezi kukutana).

وَيَوْمَ يَقُولُ نَادُوا شُرَكَائِيَ الَّذِينَ
زَعَمْتُمْ فَدَعَوْهُمْ فَلَمْ يَسْتَجِيبُوا لَهُمْ
وَجَعَلْنَا بَيْنَهُم مَّوْبِقًا ﴿٥٢﴾

53. Na wabaya watauona Moto (wakati huo) na watajua ya kwamba wao lazima wataingia humo; wala hawatapata pa kuuepuka.

وَرَأَى الْمُجْرِمُونَ النَّارَ فَظَنُّوا أَنَّهُم مُّوَاقِعُوهَا
وَلَمْ يَجِدُوا عَنْهَا مَصْرِفًا ﴿٥٣﴾

54. Na bila shaka tumewaelezea watu namna kwa namna katika hii Qurani kila mfano. Lakini mwanadamu amekizidi kila kitu kwa ubishi.

وَلَقَدْ صَرَّفْنَا فِي هَٰذَا الْقُرْآنِ لِلنَّاسِ مِن كُلِّ
مَثَلٍ ۚ وَكَانَ الْإِنسَانُ أَكْثَرَ شَيْءٍ جَدَلًا ﴿٥٤﴾

55. Na hakikuwazuia watu hawa kuamini ulipowajia uwongofu na kuomba maghufira kwa Mola wao isipokuwa (wanangoja) iwajie hali ya (wale watu) wa kwanza au adhabu jahara hivi.

وَمَا مَنَعَ النَّاسَ أَن يُؤْمِنُوا إِذْ جَاءَهُمُ الْهُدَىٰ
وَيَسْتَغْفِرُوا رَبَّهُمْ إِلَّا أَن تَأْتِيَهُمْ سُنَّةُ
الْأَوَّلِينَ أَوْ يَأْتِيَهُمُ الْعَذَابُ قُبُلًا ﴿٥٥﴾

56. Na hatuwaleti Mitume ila wawe watoaji wa khabari njema na waonyaji. Na wale waliokufuru wanajadili (wanashindana) kwa mambo yasiyokuwa na haki ili kwa mambo hayo waibatilishe haki. Na wanazifanya Aya zangu na yale waliyoonywa kuwa ni mzaha.

وَمَا نُرْسِلُ الْمُرْسَلِينَ إِلَّا مُبَشِّرِينَ وَمُنذِرِينَ ۚ
وَيُجَادِلُ الَّذِينَ كَفَرُوا بِالْبَاطِلِ لِيُدْحِضُوا
بِهِ الْحَقَّ ۖ وَاتَّخَذُوا آيَاتِي وَمَا أُنذِرُوا هُزُوًا ﴿٥٦﴾

57. Na ni nani dhalimu mkubwa kuliko yule anayekumbushwa Aya za Mola wake akawa anazipuza, na akayasahau (mabaya) yaliyotangulizwa (yaliyofanywa) na mikono yake? (Kama kwamba) sisi tumetia nyoyoni mwao vifuniko ili wasiifahamu, na kama kwamba katika masikio yao (tumetia) uzito (uziwi). Na ukiwaita katika uwongofu hawakubali abadan kuongoka.

وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّن ذُكِّرَ بِآيَاتِ رَبِّهِ فَأَعْرَضَ
عَنْهَا وَنَسِيَ مَا قَدَّمَتْ يَدَاهُ ۚ إِنَّا جَعَلْنَا عَلَىٰ
قُلُوبِهِمْ أَكِنَّةً أَن يَفْقَهُوهُ وَفِي آذَانِهِمْ وَقْرًا ۖ
وَإِن تَدْعُهُمْ إِلَى الْهُدَىٰ فَلَن يَهْتَدُوا إِذًا أَبَدًا ﴿٥٧﴾

58. Na Mola wako ndiye Mwingi wa msamaha, Mwenye rehema (pia). Kama angewatesa kwa

وَرَبُّكَ الْغَفُورُ ذُو الرَّحْمَةِ ۖ لَوْ يُؤَاخِذُهُم بِمَا

---

50. Aya hii inaonyesha kuwa Ibilisi alikuwa katika Majini, si katika Malaika kama wanavyosema wanavyuoni wengine.

53. Wanaona katika Aya hii walioifanya kuwa ni ya 54. Wanaiona inavyotaja mambo yatakayokuwa akhera. Wao wanasema ni vita vya Ulaya na Amerika. Mnawaona wapotezi hawa waovu, wanaopindua maneno ya Mwenyezi Mungu chini juu bila ya kumbali Mwenyewe Mwenyezi Mungu wanayembadilishia maneno yake.

58. Mwenyezi Mungu anawapa muda mrefu kabla ya kuwaadhibu ili wapate kutanabahi warejee.

sababu ya yale waliyoyachuma, bila shaka angewapa adhabu upesi upesi (papa hapa); lakini wanayo miadi ambayo hawatapata makimbilio yoyote ya kuepukana nayo.

59. Na miji hiyo tuliwaangamiza (wakazi wake) walipodhulumu (nafsi zao kwa mabaya) na tukawawekea miadi ya maangamizo yao (hayo).

60. Na (kumbukeni) Musa alipomwambia kijana chake: "Nitaendelea tu kwenda mpaka nifike katika maungano ya bahari mbili, au niendelee karne na karne (mpaka nikutane na huyo ninayetaka kukatana naye).

61. Basi walipofika wote wawili (mahali) zinapoungana (hizo bahari mbili) walimsahau samaki wao, naye akashika njia yake kwenda baharini, hali ya kuwa inafanya alama. (Nabii Musa alisahau kumuuliza khabari ya samaki huyo, na yule kijana alisahau kumsimulia Nabii Musa habari ya samaki huyo).

62. Na walipofika mbele (Musa) alimwambia kijana chake "Tupe chakula chetu cha asubuhi; maana tumepata uchofu (mkubwa) katika safari yetu hii (ya sasa).

كَسَبُوا لَعَجَّلَ لَهُمُ الْعَذَابَ ۚ بَل لَّهُم مَّوْعِدٌ
لَّن يَجِدُوا مِن دُونِهِ مَوْئِلًا ﴿٥٨﴾

وَتِلْكَ الْقُرَىٰ أَهْلَكْنَاهُمْ لَمَّا ظَلَمُوا
وَجَعَلْنَا لِمَهْلِكِهِم مَّوْعِدًا ﴿٥٩﴾ ع

وَإِذْ قَالَ مُوسَىٰ لِفَتَاهُ لَا أَبْرَحُ حَتَّىٰ أَبْلُغَ مَجْمَعَ
الْبَحْرَيْنِ أَوْ أَمْضِيَ حُقُبًا ﴿٦٠﴾

فَلَمَّا بَلَغَا مَجْمَعَ بَيْنِهِمَا نَسِيَا حُوتَهُمَا
فَاتَّخَذَ سَبِيلَهُ فِي الْبَحْرِ سَرَبًا ﴿٦١﴾

فَلَمَّا جَاوَزَا قَالَ لِفَتَاهُ آتِنَا غَدَاءَنَا لَقَدْ
لَقِينَا مِن سَفَرِنَا هَٰذَا نَصَبًا ﴿٦٢﴾

---

60. Inatajwa safari ya Nabii Musa kwenda kukutana na Mtume mwenziwe—Nabii Al Khidhri—ila huyu alipewa wahyi wa kuhukumu ya Batini.

60-82. Aya hizi zilizokhusu habari ya safari ndefu ya Nabii Musa kwenda kuonana na Nabii Al Khidhri, wanaisema ni njozi (ndoto), kama walivyosema mwanzo wa Sura hii, na kama walivyokifanya kisa cha Israi ya Mtume na Miiraj yake kuwa ni ndoto vile vile — si hakika. Eee ukafiri wao! Hamu yao kubwa kumsuta Mwenyezi Mungu kwa anayotwambia, wakamuona muongo, hajui hakika ya mambo! Basi kila maelezo (mapotezo) marefu marefu haya waliyoyatia chini ya Aya hizi ni uwongo kabisa; uwongo wa kweli kweli; hapana ruhusa kusadiki. Na kila wakitia uwongo wao huo wa kupoteza Waislamu kusudi, hutia—katika Bracket—*Ta-tiir-ul-Anam*. Kuwadhanisha watu kuwa wameyachukuwa maneno hayo katika kitabu madhubuti katika vitabu vya Tafsiri ya Qurani au Hadithi za Mtume — kumbe kitabu cha kufasiri ndoto kinachosema kama hivi:– kuwa ukiona msiba ndio ni furaha, ukiona mauti ndiyo uzazi. . .! Unawaona na njia zao za kishetani za kupoteza watu! Wanawadhanisha watu vingine; kumbe vingine. Nani — asiyesoma sana — atakayetambua kuwa kitabu hicho ni cha kufasiri ndoto? Ataona ni kitabu cha tafsiri ya Qurani au Hadithi Fiqh au Lugha au . . . Tuwatahadhari na dini yetu ya haki.

62. Kijana wake huyo alikuwa anafuatana naye kila mahala na akimtii kabisa. Hata mwisho wake—baada ya kufa Nabii Musa na Nabii Haruni — Mwenyezi Mungu akamfanya yeye kuwa Muongozi wa Mayahudi — Mtume wao. Na jina lake lilikuwa Yuushaa.

*N.B.* Hapa kinatajwa kisa cha Nabii Musa na Nabii Al Khidhri. Mitume hawa walikuwa wakati mmoja lakini mahala mbali mbali kabisa. Na Nabii Musa alikuwa bora zaidi kuliko huyu Nabii Al Khidhri kwa ilimu na kwa kila kitu. Lakini hwenda kikapatikana kwa aliye mdogo ambacho hanacho mkubwa. Na yamefanywa haya na Mwenyezi Mungu ili wasitakabari hao walio wakubwa. Wajijue kuwa hata wakiwa wakubwa vipi lakini upungufu wanao tu. *Al Kamaalu Lillahi.* Ukamilifu ni Wake Mwenyewe tu Mwenyezi Mungu.

Basi inasemekana ya kuwa siku moja Nabii Musa alipokuwa anawakhutubia watu akatoa ilimu kubwa, aliondoka mtu akamuuliza 'Unafikiri yuko mtu mwenye ilimu zaidi kuliko wewe'? Akasema 'Hakuna'. Basi Mwenyezi Mungu hakufurahi na msemo huu akamwambia, "Ingawa wewe una ilimu kubwa kabisa lakini yuko mja wangu mmoja, jina lake Al Khidhri, nimempa kujua baadhi ya mambo ya Batini (ya Ndani yasiyofahamika na watu); na wewe nimekupa ilimu ya mambo ya Dhahiri tu. Basi nenda ukakutane naye uone namna anavyotambua mambo ya Batini."

Basi akafunga safari pamoja na huyo mfuasi wake wakenda huko aliko Nabii Al Khidhri.

63. Akasema: "Unaona! Pale tulipopumzika katika mlima basi hapo nimesahau (kukupa habari ya) yule samaki. Na hakuna aliyenisahaulisha isipokuwa Shetani, nisikumbuke. Naye akashika njia yake baharini kwa namna ya ajabu."

قَالَ أَرَءَيْتَ إِذْ أَوَيْنَآ إِلَى ٱلصَّخْرَةِ فَإِنِّى نَسِيتُ
ٱلْحُوتَ وَمَآ أَنسَىٰنِيهُ إِلَّا ٱلشَّيْطَٰنُ أَنْ أَذْكُرَهُۥ ۚ
وَٱتَّخَذَ سَبِيلَهُۥ فِى ٱلْبَحْرِ عَجَبًا ﴿٦٣﴾

64. (Musa) akasema: "Hapo ndipo tulipokuwa tunapataka." Basi wakarudi nyuma kwa kufuata njia yao (ile ile)

قَالَ ذَٰلِكَ مَا كُنَّا نَبْغِ ۚ فَٱرْتَدَّا عَلَىٰٓ ءَاثَارِهِمَا
قَصَصًا ﴿٦٤﴾

65. Basi wakamkuta mja katika waja wetu (Sisi Mwenyezi Mungu) tuliyempa rehema kutoka kwetu na tuliyemualimisha ilimu (nyingi) zinazotoka kwetu.

فَوَجَدَا عَبْدًا مِّنْ عِبَادِنَآ ءَاتَيْنَٰهُ رَحْمَةً مِّنْ
عِندِنَا وَعَلَّمْنَٰهُ مِن لَّدُنَّا عِلْمًا ﴿٦٥﴾

---

Na haijulikani kwa hakika ni mahala gani khasa katika hii dunia yetu. Wengine wanasema katika miji ya pwani ya Persian Gulf au Red Sea au Mediterranean Sea ambapo bahari hizi zinakutana hapo na hizo bahari zinazopakana nazo.

63. Alama aliyopewa Nabii Musa ya kumfahamisha kuwa mahala hapo ndipo atakapokutana na huyo Al Khidri ni kuwa samaki wake aliyekwisha kupikwa atafufuka atoke kikapuni endezake baharini.

Basi walipofika mahala fulani karibu na bahari wakatua hapo kupumzika, Nabii Musa alilala kidogo, na yule mtoto alikuwa yumacho. Mara akamuona yule samaki aliyekwisha kupikwa anatoka kikapuni anafuata njia katika ufuko wa pwani na huku inafanya alama hiyo njia anayopita, mpaka akaingia baharini.

Akasema moyoni mwake kuwa akiamka Nabii Musa nitampa habari ya ajabu, lakini alisahau. Alipoamka Nabii Musa, hao wakaondoka wanazidi kwenda mbele. Hata baada ya kufika mbali; ukawa wakati wa kula. Nabii Musa akataka chakula, hapo ndipo yule mtoto alipokumbuka akamjuvya Nabii Musa habari ile.

Basi Nabii Musa akamwambia warejee huko ulipotokea muujiza huo kwani hapo ndipo watakapomkuta huyo wanayemtafuta.

Basi wakarejea kwa njia ile ile; na walipofika hapo wakamkuta huyo Nabii Al Khidri; yakatokea hayo tuliyosimulia.

Lakini tafsiri ya vitendo hivyo alivyovifanya Nabii Al Khidri vitasimuliwa katika juzuu ya 16 inayofuatia juzuu hii. Hapa utaona mshangazo lakini ukishakuona tafsiri yake utakutoka mshangao huu.

65. Katika aya waliyoifanya ya 66 wamezidi kupoteza wakasema:– "Mtumishi wa Mungu ambaye Nabii Musa alimfungia safari hii ya kumtafuta si mwingine ghairi ya Mtume Muhammad . . . ndiye *abd* anayetajwa katika kisa hiki." Wanajua — kwa Hadithi za Mtume sahihi zilizomo katika Al Bukhary na kwingineko — kuwa Mtume aliyekusudiwa hapa ni Nabii Al Khidri. Wanajua kwa yakini lakini wanataka kupoteza tu. Wanasema kuwa tamko la Abd ndilo lililowadhihisha hapa kuwa amekusudiwa Nabii Muhammad. Wakataja Aya za Qurani zilizotaja *Abd,* ikawa makusudio yake ni Nabii Muhammad. Na nyingine katika hizo si makusudio yake Nabii Muhammad—kama ya 39: 36; lakini basi tu wamepachika. Na wanajua yakini kuwa Mwenyezi Mungu amewatumilia Mitume wengine pia tamko la *Abd* na *Ibad,* kama *Abdahuu Zakariyya* (Aya ya 2 ya *Surat Maryam*). *Abdanaa Daawuud* (Aya ya 17 ya *Surat Sad*). *Abdana Ayyub* (Aya ya 41 ya *Surat Bani Israil*). *Tahta Abdayni (Nuhu na Luti,* Aya ya 10 ya *Attahrym*). *Ibaadanaa Ibrahima, Wa Is-haaqa wa Yaaquuba. . .* (Aya ya 45 ya *Sad*). Na Mitume wengine pia wametumiliwa hivi, bali hata wema wengine pia wasiokuwa Mitume wametumuliwa tamko hili, kama *Waibaadur Rahman* iliyoko katika Aya ya 63 *Suratul Furqan,* na chungu nyinginezo. Wanajua, lakini wanataka tu kupotoa muradi wa Mwenyezi Mungu — kama kwamba Mwenyezi Mungu ni adui yao, wanataka kumharibia kila lake, la maneno na vitendo!

Na hoja yao ya pili waliyotoa ya kudanganya kuwa hapa amekusudiwa Nabii Muhammad ni kusema kwao: "Maneno haya, Tuliyempa Rehema, ni wazi yamhusu Mtume Muhammad. Yeye peke yake ameitwa katika Qurani Rehema kwa walimwengu, (Sura 21:108)." Tazama kujitia pambani kwao! Haikuambiwa hapa "Anaitwa Rehema." Imeambiwa "Tumempa rehema." Na Mwenyezi Mungu amewatajia chungu ya Mitume kuwa amewapa rehema; bali na hata wasiokuwa Mitume. Katika Mitume ni Nabii Ibrahimu; kama ilivyo katika Aya ya

66. Musa akamwambia: "Je! Nikufuate ili unifundishe katika ule uwongofu (uwongozi) uliofundishwa?"

قَالَ لَهُۥ مُوسَىٰ هَلْ أَتَّبِعُكَ عَلَىٰٓ أَن
تُعَلِّمَنِ مِمَّا عُلِّمْتَ رُشْدًا ﴿٦٦﴾

67. Akasema: "Hakika wewe huwezi kuvumilia kuwa pamoja nami. (Utaona usiyoweza kustahimili kuyaona)."

قَالَ إِنَّكَ لَن تَسْتَطِيعَ مَعِىَ صَبْرًا ﴿٦٧﴾

68. "Na utawezaje kuvumilia yale usiyoyajua hakika yake?"

وَكَيْفَ تَصْبِرُ عَلَىٰ مَا لَمْ تُحِطْ بِهِۦ خُبْرًا ﴿٦٨﴾

69. Akasema: "Akipenda Mwenyezi Mungu, utaniona mvumilivu, wala sitaasi amri yako."

قَالَ سَتَجِدُنِىٓ إِن شَآءَ ٱللَّهُ صَابِرًا وَلَآ أَعْصِى
لَكَ أَمْرًا ﴿٦٩﴾

70. Akasema: "Basi kama utanifuata, usiniulize kwa lolote (utakaloliona), mpaka mimi nianze kukwambia."

قَالَ فَإِنِ ٱتَّبَعْتَنِى فَلَا تَسْـَٔلْنِى عَن شَىْءٍ
حَتَّىٰٓ أُحْدِثَ لَكَ مِنْهُ ذِكْرًا ﴿٧٠﴾

71. Basi wote wawili wakaondoka (wanakwenda). Hata walipopanda jahazi (yule Nabii Al Khidhri) aliitoboa. (Musa) akasema, "Je! umeitoboa ili uwazamishe waliomo? Hakika umefanya jambo baya."

فَٱنطَلَقَا حَتَّىٰٓ إِذَا رَكِبَا فِى ٱلسَّفِينَةِ خَرَقَهَا ۖ
قَالَ أَخَرَقْتَهَا لِتُغْرِقَ أَهْلَهَا لَقَدْ جِئْتَ
شَيْـًٔا إِمْرًا ﴿٧١﴾

72. Akasema: "Je! Sikusema kuwa wewe hutaweza kuvumilia kuwa pamoja nami?"

قَالَ أَلَمْ أَقُلْ إِنَّكَ لَن تَسْتَطِيعَ مَعِىَ صَبْرًا ﴿٧٢﴾

73. (Musa) akasema: "Usinipatilize (usinitie adabu) kwa kule kusahau kwangu, wala usinitie katika tashdidi kubwa (taabu) kwa jambo langu (hili la kufuatana nawe)."

قَالَ لَا تُؤَاخِذْنِى بِمَا نَسِيتُ وَلَا تُرْهِقْنِى
مِنْ أَمْرِى عُسْرًا ﴿٧٣﴾

74. Basi wote wawili wakaendelea kwenda. Hata wakamkuta kijana mdogo, na (yule Al Khidhri) akamuua. (Musa) akasema: "Ala! Umemuua mtu asiye na kosa wala hakumuua mtu? Bila shaka umefanya jambo baya kabisa."

فَٱنطَلَقَا حَتَّىٰٓ إِذَا لَقِيَا غُلَٰمًا فَقَتَلَهُۥ قَالَ أَقَتَلْتَ
نَفْسًا زَكِيَّةًۢ بِغَيْرِ نَفْسٍ لَّقَدْ جِئْتَ شَيْـًٔا نُّكْرًا ﴿٧٤﴾

---

73 ya *Surat Hud,* na Mitume wenziwe waliotajwa katika hiyo *Surat Hud* na nyinginezo Na wasiokuwa Mitume ni hao waliotajwa katika Aya ya 157 ya *Suratul Baqarah* na nyinginezo. Bali hata kuambiwa Mtume Muhammad kuwa yeye mwenyewe huyo ni rehema, hakuambiwa Nabii Muhammad pia peke yake, bali aliambiwa Nabii Isa pia kama ilivyo katika Aya ya 21 ya *Surat Maryam,* bali na wengineo pia; wala hayakhusu kitu haya kwani huyo Nabii Al Khidhri hakuambiwa yeye ni rehema, bali imeambiwa amepewa rehema. Uwongo wao unafedheheka tu. Na kila usiko uchao utazidi kufedheheka.

Na hoja yao ya tatu ya kusema kuwa huyo ni Nabii Muhammad ni kusema: "Maneno Tuliyemwelimisha elimu kutoka kwetu pia yanamhusu Mtume Muhammad s.a.w. mahala pengi katika Qurani imesemwa amepewa elimu kwa kadiri kubwa sana (Sura 4:114, 6:92, 20:115; 27:7)." Uwongo. Waongo Makadiyani. Sura 4:114 haikusema hivyo; wala 6:92 wala 20:115 wala 27:7 pia. Tazama uzushi wao walivyozisingizia hizi Sura hapa na Aya. Wao wanajua kuwa hakuna atakayefunua vitabu akatazama. Ndipo maana wakawa wanasukuma tu watakavyo. Na Mitume wote wameambiwa wamepewa Ilimu. Basi ikiwa Aya hii ya 65 ya *Suratul Kahf* inamrejelea Nabii Al Khidhri pana makosa gani?

69-74. Wameendelea kusema kuwa mambo hayo yote ni ndoto, na wakatoa tafsiri za uwongo za tafsiri yao hiyo ya uwongo ya ndoto, na wakazalisha humo uwongo juu ya uwongo, ikaja humo farumu ya uwongo.

Waongo waongo — Wao daima waongo
Wamekiuka mpaka — Katika wao uwongo